
SportPesa
TZS. 783,781,040
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Kanisa lawakataza wanawake kwenda kliniki, watoto shule**

UKURASA 4



**PSG, Real Madrid zamwania Rudiger**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Desemba 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580796

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Rais Samia: Niko tayari kusamehe

• **Ataka** kuanza ukurasa mpya, wanasiasa kusahau yaliyopita, Zitto ataka aliyeko ndani atolewe, CHADEMA yatia neno... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### MAELEZO ONYO YASOMWA KESI YA FREEMAN MBOWE

MSHTAKIWA wa tatu, Mohemmed Ling'wenya, katika maelezo yake ya onyo inadaiwa alimtaja Luteni Dennis Urio...

## Waziri apiga marufuku DED kushusha vyeo walimu wakuu

UKURASA 3



Gari aina ya Toyota Land Cruiser VX V8 lenye namba za usajili T222 DBY, linalodaiwa kununuliwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, likiwa katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana, kama kielelezo cha ushahidi katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili Sabaya na wenzake sita. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Gari analodaiwa kuuziwa Sabaya lafikishwa kortini

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA YATOA SABABU USHINDI KIDUCHU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Wahasibu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), wakiwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa shtaka la kuingiza data za uwongo kwenye mfumo wa malipo na kuisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. milioni 600. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia: Niko tayari kusamehe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hakuna mtu mwenye cheti cha umiliki wa nchi ya Tanzania, huku akiwataka wanasiasa kusahau yaliyopita na kuzika tofauti zao na yeye yuko tayari kusamehe na kuanza upya kwa maslahi mapana ya taifa.

Rais pia ameliagiza Jeshi la Polisi na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kukaa pamoja na wadau wa demokrasia nchini kujadiliana namna bora itakayotumiwa na vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara bila kuvunja sheria za nchi.

Rais Samia alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipofungua mkutano wa wadau wa kujadili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

"Nikuombeni tusitizame yaliyopita, tuangalie mbele Tanzania mpya yenye kuheshimiana. Niko tayari kusikiliza, kukosolewa na pia nipo tayari kusamehe na nyie pia muwe tayari kufuata sheria.

"Ninajua ipo bado dukuduku, nongwa, malalamiko ambayo yanatokana na uchanga wa demokrasia ya nchi yetu," alisema.

Rais pia alisema serikali yake iko tayari kupokea maoni kwa ajili ya kuboresha Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na mambo yanayoshabihiana nayo ili kuimarisha demokrasia nchini.

"Tuko tayari kupokea maoni ya vyama vya siasa ambayo yataletwa kwetu kwa utaratibu na kuyafanyia kazi ili kuboresha demokrasia ya nchi yetu na pale inapotokea maoni yako kukataliwa, isiwe sababu ya wewe kufanya vitu ambavyo vinaashiria uvunjifu wa sheria za nchi, kuna msemo unasema 'wengi wape'," alisema.

Kuhusu kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini, Rais Samia alisema ni haki yao kisheria na kikatiba, lakini hivi sasa wamezuiliwa kutokana na wengi wao kufanya mambo yanayoashiria uvunjifu wa sheria.

"Ninawaombeni mfuate Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja ile nyingine ambayo inatoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kufanya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini.

"Kila jambo lina utaratibu wake lakini sivyo ambavyo kama mmekuwa mkifanya vitendo vya fujo na kutishia kutoweka kwa amani," alisema.

Rais alisema viongozi wa siasa siyo watoto wadogo ambao wanashindwa kusimamia sheria hadi wafungiwe kufanya mikutano yao kwa kukiuka miongozo ya nchi.

"Sheria lazima tuzifuate, hatuwezi kufanya mambo kiholela, nyie (ninyi) sisi watoto wadogo hadi mfungiwe, wanafunzi ndiyo wanafungiwa, lakini si ninyi, hivyo niwaombe sana kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinafuta sheria," aliagiza.

Rais Samia alimwagiza Msajili wa Vyama vya Siasa kutumia mkutano huo kukaa pamoja na Jeshi la Polisi na wadau hao ili kujadiliana namna sahihi ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara bila ufunjifu wa sheria.

"Mkae mjifungie wenyewe na mapendekezo hayo muyalete kwetu, sisi tutapitia na tukiona yanafaa tutaruhusu mikutano ya hadhra lakini tukiona bado kuna upungufu, hatutaruhusu," alisema.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuutumia mfumo wa vyama vingi kama sehemu ya kuwapa wananchi mbadala wa nini watafanya kusaidia maendeleo ya nchi.

"Siasa siyo matusi, siyo kuchafuana, siyo kuchonganisha wananchi na serikali yao, lakini siasa siyo ugomvi, siasa inatumika kama sehemu ya kuleta maendeleo na fikra tofauti katika kusaidia kujenga taifa.

"Kuna watu wanasema kuwa mtu anayesema uongo ni mwanasiasa lakini siasa siyo uongo," Rais Samia alisema. Akizungumzia hotuba hiyo ya Rais, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema imefungua ukurasa mpya kwa wanasiasa wa Tanzania.

Prof. Lipumba alisema hotuba hiyo imetoa mwanga wa kupatikana kwa maridhiano ya kisiasa ambayo vyama va siasa vilikuwa vinayatarajia kwa muda mrefu.

"Hotuba hii imeleta mwanga katika maridhiano, lakini demokrasia iliyokuwa inaonekana kwa muda mrefu kukandamizwa, sasa inakwenda kupata nguvu katika taifa letu," alisema.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema anakubaliana na Rais Samia kwamba mikutano ya hadhara ni haki ya kikatiba na kisheria kwa vyama vya siasa, hivyo viachwe vifanye shughuli zake kwa mujibu wa sheria na kanuni hizo.

"Ni wakati wa kuhakikisha kila mmoja anafuata sheria. Jeshi la Polisi lifuate sheria, vyama vifuate sheria, watumishi wa serikali nao wafuate sheria.

"Kila mmoja akifuata sheria, ninaamini hakutakuwa na tatizo lolote la vyama kuingiliwa kufanya shughuli zake za kisiasa," alisema.

Mkazi wa Mtaa wa Swaswa jijini Dodoma, Hamis Sharif, alisema hotuba ya Rais imekuwa na matumaini makubwa hasa kwa wadau wa masuala ya siasa na demokrasi nchini.

Alisema matumaini hayo ameyaona pale Rais Samia alipozungumzia umuhimu wa kuruhusu mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa.

## 'Kilio' cha Zitto kwa Rais Samia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kituo cha Demokrasia nchini (TCD) na Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuliunganisha taifa kuwa kitu kimoja kutokana na kile alichokiita kuparaganyika kwa kiasi kikubwa.

Mwanasiasa huyo alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza katika ufunguzi wa mkutano wa wadau wa kujadaili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

"Ninashukuru kwa kupata nafasi hii kwani sijaongea siku nyingi sana na mbele ya Rais na imekuwa ghafla sana kwangu, lakini Mweshimiwa Rais, sisi tunachukulia nafasi hii ya mkutano huu kama sehemu ambayo itafungua mjadala wa masuala ya kisiasa nchini.

"Kwa utaratibu huu wa majadiliano ambao tunatoa changamoto zetu na ndiyo taratibu zetu Watanzania," alisema.

Vilevile, alimwomba Rais kuwaunganisha Watanzania walioparaganyika kutokana na tofauti mbalimbali ikiwamo za kisiasa ili kulifanya taifa kuwa moja.

"Mama tunakuomba utuunganishe Watanzania, hivi sasa tumeparaganyika sana na tuna imani kuwa uwezo huo unao. Sisi leo tupo hapa na wengine hawapo kwa sababu zao wanazozijua wao.

"Mwenzetu mmoja yupo ndani kwa sababu za kisheria, tunakuomba mwenzetu huyo uone namna ya kufanya tuwe naye, atoke tuje kufanya naye siasa," aliwasilisha ombi lao.

Katika hotuba yake, Rais Samia alipokea ombi hilo, akisisitiza kuwa demokrasia siku zote ni kuheshimu sheria.

"Heshima ya mtu inakuja kwa kuheshimu sheria. Unapotumia uhuru wako ujue mwisho wa uhuru wako ndiyo mwanzo wa uhuru wa mtu mwingine. Ninaomba tufanye kazi kwa kuheshimu sheria, kuna msemo unasema mtaka nyingi na saba hupata mwingi msiba japokuwa kusameheana pia kupo," Rais Samia alisema.

Mkuu wa nchi alisema vyama vya siasa pamoja na asasi za kiraia vinatakiwa kufuata na kuzingatia sheria za nchi ili amani iendelee kutamalaki.

"Hakuna jambo linalokosa kasoro, lakini tukikaa pamoja na kujadiliana, tutaondoa kasoro zetu," alisema.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema mkutano huo ni ishara tosha kuwa serikali chini ya Rais Samia inatambua umuhimu wa demokrasia nchini.

"Mheshimiwa Rais uwapo wako hapa leo ni ishara tosha kuwa serikali yako inatambua umuhimu wa demokrasia nchini," alisema.

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mtungi, alisema lengo la mkutano huo ni wadau wa demokrasia nchini kukaa pamoja na kujadili kero mbalimbali na kuzipatia majibu.

Alisema mkutano huo pia utasaidia vyama vya siasa nchini kuzingatia sheria na kwa wale wenye maoni yao kuyawasilisha kwa utaratibu ili yapatiwe majibu.

"Mheshimiwa Rais hadi sasa ofisi yangu imesajili usajili wa kudumu kwa vyama 19 vya siasa ambavyo ndivyo vilishiriki uchaguzi mkuu mwaka jana kutoka vyama 13 mwaka 1995," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Ali Khatibu, alimpongeza Rais Samia kwa kazi anazozifanya ikiwa ni pamoja na kufungua ushirikiano na mataifa mengine duniani.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa siku tatu wa wakuu wa shule za sekondari nchini unaoratibiwa na Kampuni ya Global Education Link (GEL) na Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSSA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ummy awashukia Ma-DED kushusha vyeo walimu wakuu

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imepiga marufuku tabia ya wakurugenzi wa halmashauri nchini kuwashusha vyeo walimu wakuu wa shule pindi shule zao zinapopata matokeo mabaya.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, wakati akifungua mkutano wa wakuu wa shule za sekondari nchini katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Mkutano huo wa siku tatu umeratibiwa na Global Education Link (GEL) kwa kushirikiana na Umoja wa Walimu Wakuu Shule za Sekondari (TAHOSSA).

Ummy alisema inashangaza kuona walimu wakuu wakishushwa vyeo holela na wakurugenzi kila shule inapofanya vibaya wakati mwalimu huyo hajawezeshwa.

"Walimu mmekuwa msaada mkubwa sana kwa maendeleo ya elimu lakini hii tabia ya kuwaonea kwa kuwashusha vyeo imeshamiri na siikubali. Sasa kuanzia leo (jana) sitaki kusikia tabia hii nitawalinda walimu wangu dhidi ya unyanyasaji wa mtu yeyote," alisema Ummy

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy alisema shule zote mpya zinazojengwa na serikali zitakuwa na maabara za komyupta na vifaa vyote vinavyohitajika ili kuwezesha masomo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Alisema katika mpango wa miaka mitatu kuanzia mwakani, serikali inapanga kuanza na shule 1,500 ziwekwe maabara ya kompyuta zenye vifaa vyote muhimu.

Waziri Ummy alisema katika mpango huo, serikali imepanga kuweka kompyuta 50 kila shule zikiwa na vifaa vyote vya TEHAMA na kwamba mpango wa muda mrefu ni kuhakikisha shule zote za serikali zinakuwa na maabara za kompyuta.

Pia Waziri Ummy alipiga marufuku michango holela shuleni ambayo imekuwa kero kwa wazazi na kwamba ambao hawatasikia agizo hilo watachukuliwa hatua kali ili iwe mfano kwa wengine.

"(Hayati Rais John) Magufuli alipiga marufuku michango kama hii na Rais Samia (Suluhu Hassan) ameendeleza elimu bure na serikali yake imekataza michango lakini haiishi. Waacheni wanafunzi wajiunge na shule hata kama hawana sare kwani bila sare hafundishiki?" alihoji

"Katibu mkuu tutoe mwongozo michango ya lazima ni ipi ili iwe wazi mtoto akianza kidato cha kwanza awe na nini maana bila hii miongozo wengine wataendeleza hii tabia tumesema sana lakini naona kuna watu hawasikii," alisema

Waziri alisema walimu wanapaswa kuwa walezi na washauri bora wa wanafunzi hivyo wasiwe sehemu ya kundi ovu linaloharibu wanafunzi.

Kuhusu masomo ya ziada, Ummy alisema serikali inachokataza ni masomo ya ziada ya lazima ambayo wanafunzi wamekuwa wakilazimishwa kulipia wakati wa likizo.

"Kama unataka kufanya masomo ya ziada wakati wa likizo fuata utaratibu kwa sababu kanuni na miongozo kuhusu hilo ipo ifuate kwa kuomba kibali sehemu husika badala ya kila mmoja kufanya holela holela na mwanafunzi apewe muda wa kutosha wa kupumzika," alisema.

# Gari analodaiwa kuuziwa Sabaya lafikishwa kortini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

GARI aina ya Toyota Landcruiser VX V8, lenye usajili T222 DBY linalodaiwa kununuliwa na aliyekuwa Mkuu wa wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, limefikishwa mahakamani na shahihi wa 12 wa Jamhuri, Sharif Shahib (36), kuomba lipokewe kama kielelezo cha ushahidi.

Gari hilo lenye rangi ya kijivu, lilifikishwa jana katika viwanja vya mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda, likiwa limeshehi nguo na viatu vilivyokuwa kwenye buti.

Shahidi huyo ambaye ni mfanyabiashara wa magari Ilala jijini Dar es Salaam, ndiye aliyedaiwa kumuuzia Sabaya gari hilo na aliomba lipokewe kama kilelelezo.

Sabaya na wenzake sita, wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi. Wengine ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Baada ya ombi la shahidi huyo, mahakama ilipokea gari hilo kama kielelezo cha ushahidi na mawakili wa upande wa utetezi hawakuwa na pingamizi la gari kupokewa. Pia shahidi alikabidhi funguo za gari mahakamani.

Awali akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, shahidi huyo alidai kwamba Aprili 16, mwaka huu, alipata kadi kutoka kwa wakala wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kubadili umiliki wa gari hilo kwenda kwa Ole Sabaya.

Pia alidai kwamba baada ya kukabidhiwa kadi hiyo, alimjulisha Sabaya na kumtumia kwa njia ya WhatsApp na kwamba tarehe ya kutuma kadi ya gari kwenda kwa Sabaya, inatofautiana na ile ambayo alikabidhiwa na wakala wa TRA.

Shahidi huyo alidai kwamba Juni Mosi, mwaka huu, majira ya saa 6:00 mchana, alipigiwa simu kufika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) makao makuu kwa ajili ya kutoa maelezo ya biashara ya gari waliyofanya na Sabaya.

Akihojiwa mahakamani hapo, alidai kwamba aliuza gari hilo kwa kiongozi huyo wa zamani kwa thamani ya Sh.milioni 60.

"Biashara ya gari tulifanya Februari 2, mwaka huu, katika eneo letu la kuuzia magari," alidai shahidi.

Alidai kuwa kabla ya kuuza kwa Sabaya, alimuuzia mtu anayeitwa Filikunjombe kwa Sh. milioni 90 na alitoa Sh. milioni 70 na kiasi kilichobaki cha Sh. milioni 20 alishindwa kulipa.

"Baada ya Filikunjombe kushindwa kulipa kiasi cha fedha kilichobakia alianza kutangaza kwenye mitandao ya kijamii na kupitia kwa madalali ndipo Sabaya akaona naliuza," alidai shahidi.

Alidai kuwa Februari 2, walikutana na Sabaya katika apartment ya 'Black Hood' iliyopo kijitonyama jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kwenda na nyaraka za hati miliki ya gari kwa ajili ya kufanya biashara.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS tbs

**ISO 9001:2015 Certified**

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATAPELI WANAOCHUKUA BIDHAA ZA WAFANYABIASHARA**

**Dar es Salaam, 15 Disemba 2021**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linawataarifu wafanyabiashara kuwa hivi karibuni kumekuwa na kundi la watu ambao ni matapeli wanaojitambulisha kuwa ni wafanyakazi/wakaguzi wa TBS na kukagua maduka yanayouza bidhaa za chakula na vipodozi. Matapeli hao hukamata, huchukua bidhaa na kuwaagiza wafanyabiashara kufuata bidhaa hizo TBS kwa maelezo na hatua zingine za kisheria.

TBS inawakumbusha wafanyabiashara kuwa ni haki yao ya msingi kuhakiki uhalali wa zoezi la ukaguzi kwa kufanya mawasiliano na Shirika ili kujiridhisha na uhalali wa zoezi hilo na mkaguzi aliyemtembelea kwa kutumia mawasiliano yafuatayo;

**0800 11 0827** Namba ya Bure Kituo cha Huduma kwa Wateja.
**0719 220 696** Athumani Kissumo (Mkuu wa Ukaguzi na Ufuatiliaji)

**Imetolewa na:**

**Gladness H Kaseka**
**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko**

# Kanisa lawakataza wanawake kliniki

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

UKISTAAJABU ya Musa utaona ya Firauni. Ndivyo unavyoweza kusema, baada ya kanisa moja la kigeni kudaiwa kuwazuia wajawazito katika kata ya Nanjara, wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro kwenda kliniki kupata huduma za uchunguzi, kujifungulia hospitalini, kutumia dawa tiba na watoto kwenda shule!

Pia inadaiwa kuwa waumini au wafuasi wa Kanisa la Akorino, ambao ni wanawake waliofiwa na waume zao, hawaruhusiwi kuolewa na mtu mwingine zaidi ya kutafutiwa mwanamume ambaye ni muumini wa kanisa hilo.

Jana, baadhi ya wakazi wa kata za Nanjara na Ubetu Kahe katika wilaya ya Rombo, kwa nyakati tofauti walieleza namna wasivyofurahishwa na imani hiyo, huku wakiiomba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kufanya uchunguzi wa kina juu ya dhehebu hilo na kuchukua hatua stahiki ili kulinda ustawi wa wananchi wa maeneo hayo.

Mwanaharakati Beatrice Jackob, mkazi wa Nanjara alisema: "Hilo Kanisa la Wakorino limetokea nchi jirani (Kenya) na hivi sasa limeanzishwa na lipo eneo la Kibaoni, kata ya Nanjara. Linazuia wajawazito kwenda kliniki ama kwenda hospitali au watoto kwenda shule.

"Au ukiumwa unafanyiwa maombi na sio kwenda hospitali na kumeza dawa yeyote. Inatushangaza kwa sababu kuna mjamzito alikuwa na mumewe mgonjwa, hakwenda hospitali wakasema wanafanyiwa maombi mpaka akafariki. Hilo kanisa bado lipo na linaendelea kufanyia maombi nyumbani kwa mtu mmoja pale Nanjara." Malalamiko hayo yaliibuliwa wakati wa mafunzo ya siku mbili ya watendaji kata, viongozi wa dini, wanawake, vijana, maofisa maendeleo ya jamii na viongozi wa mila wa kata za Nanjara, Mrao Keryo na Ubetu-Kahe,kuhusu uongozi, utawala bora na ukatili wa kijinsia yanayoendeshwa na Shirika la kiraia la KWIECO) kupitia mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja katika kutetea haki za wanawake

Mchungaji, Donath Tarimo wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God, alisema: "Na mimi nashangaa kwa sababu hakuna dhehebu lolote katika Biblia lililowahi kuwakataza watoto wasiende shule. Nawaza tu kwenye imani hiyo yapaswa serikali ichukue hatua."

Mmoja wa wazee wa mila, Daudi Silayo, alisema: "Mtu akifariki dunia kulingana na imani ya wanaosali katika kanisa hilo, tumeona juzi juzi, ukifa wanazika siku hiyo hiyo kama umefariki mapema, na juu ya kaburi wanalikanyaga na kuotesha migomba, hawataki kuwe na alama ya kaburi. Ukipita hapo huwezi kujua kama kuna mtu amezikwa."

Mwanaharakati na Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Nguvu ya Pamoja katika Kutetea Haki za Wanawake na Watoto na Kupambana na Ukatili wa Kijinsia mkoani Kilimanjaro, Veronica Ollomi, alisema kuzuia wanawake kwenda kujifungulia hospitalini, kuzuia watu kupata huduma za afya ni kosa kisheria na ni ukatili dhidi ya binadamu. "Wakati wa majadiliano tumebaini kwamba viko vitendo vya ukatili wa kijinsia vinaendelea ndani ya jamii Rombo, ambavyo kwa kiasi kikubwa havisemwi. Kuna suala la dhehebu la Wakorino ambalo linakataza watu hasa wajawazito kwenda hospitali.

Alipoulizwa kuhusu taarifa hizo, Ofisa Mtendaji wa kata ya Nanjara, Matei Severini, alisema: "Nimezisikia hizo taarifa za hilo Kanisa la Wakorino, nimejisikia vibaya na kwa kweli imenishangaza sana kwa sababu hiyo taarifa nilikuwa sina, na nilivyoipata nimejifunza kitu, nimepata pa kuanzia, naamini hilo suala litaisha."

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Rombo, Consolatha Massawe, alisema kinachosikitisha ni kwamba wakati hayo yote yanatokea, viongozi wa eneo husika wapo na hawajachukua hatua au kutoa taarifa ngazi ya wilaya.

"Tuko ndani ya jamii ya Rombo, kule hayo yote yanayotokea viongozi wapo, zaidi sana kuna yale majukwaa, kuna zile Kamati za Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), ziko ndani ya eneo husika na watendaji wako ndani ya eneo husika."alisema

"Ofisa Tarafa yuko eneo husika, Mtendaji wa Kata, kuna Mtendaji wa Kijiji, kuna wazee mashuhuri, halafu pia kuna watu wanaweza wakasaidia kwa njia moja au nyingine. Kinachosababisha tunafika hapo ni ile jamii inayozunguka hilo eneo kutotoa taarifa kwa wahusika ili hao watu wafuatiliwe na hatua ziweze kuchukuliwa dhidi yao.



Mfanyakazi wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Tudar Mwasyeba, akijifunza kuzima moto wakati wa mafunzo ya utayari wa kukabiliana na majanga yaliyoendeshwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kinondoni, kwa wafanyakazi wa TGL, mkoani Dar es Salaam juzi. Wapili kulia ni Mkufunzi wa mafunzo hayo, Sajini Aman Hassan. **PICHA: SANULA ATHANAS**

## Maelezo ya onyo yasomwa kortini kesi ya kina Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MSHTAKIWA wa tatu, Mohemmed Ling'wenya, katika maelezo yake ya onyo inadaiwa alimtaja Luteni Dennis Urio kwamba alimtafutia kazi kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na aliwaambia wadai mshahara wa Sh. 800,000 kila mmoja.

Ling'wenya anadaiwa kudai hivyo, lakini mshtakiwa wa pili Adamu Kasekwa katika maelezo yake yaliyopokewa kama kielelezo mahakamani, alimtaja Luteni Urio kuwa alimtafutia kazi kwa Mbowe.

Maelezo hayo ya onyo ya Ling'wenya yalisomwa jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na SP Jumanne Malangahe mbele ya Jaji Joachim Tiganga baada ya mahakama kuyapokea kama kielelezo cha upande wa Jamhuri.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, SP Jumanne alidai mshtakiwa Ling'wenya alimpa haki zake zote na katika maelezo ya onyo alikiri kuonywa na kupewa haki zake zote kisha kutia saini.

Anadai mshtakiwa katika maelezo ya onyo alikiri kula njama kufanya matendo ya kigaidi, alitaka kushiriki kukata miti na kuweka magogo barabarani.

Inadaiwa shughuli ya kuhamasisha vurugu zilitakiwa kufanyika kabla ya Agosti 12, mwaka 2020 na wao walikamatwa Agosti 5, mwaka huo. Katika maelezo yake, alidai kuwa Julai 2020 alipigiwa simu na aliyekuwa mwalimu wake Kikosi cha 92 KJ Ngerengere, Luteni Deniss Urio, alimwambia kuna kazi amemtafutia.

Alidai alikwenda na mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, Morogoro kuonana na Luteni Urio, ambaye aliwaambia kuna kazi ya ulinzi wa kiongozi kwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

"Luteni Urio alituambia tuombe mshahara wa Sh. 800,000, aliongea na baba yangu kuhusu hiyo kazi wakakubaliana, tulirudi Morogoro kwa pikipiki hadi Chalinze kisha tukaanza safari ya Moshi," ilidaiwa katika sehemu ya maelezo yake ya onyo.

Alidai kuwa walikwenda Moshi na Kasekwa, walifika Aishi Hoteli ambako walikutana na Mbowe, akiwahoji kama wanaijua siasa, walijibu hawaijui.

Inadaiwa katika maelezo hayo kuwa Mbowe aliwaambia aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, anamsumbua, anatakiwa apigwe ili kumpunguzia nguvu lakini asiuliwe.

Anadai katika mazungumzo yao walikubaliana mshahara huo wa Sh. 800,000, Mbowe aliwapa fedha ya maandalizi sababu siku iliyokuwa inafuata kulikuwa na kazi ya kumpokea Tundu Lissu.

Shahidi aliomba kutoa hati ya kukamata mali za washtakiwa iwe sehemu ya ushahidi wake lakini upande wa utetezi walipinga kupokewa kwa kielelezo hicho kwa sababu mbalimbali za kisheria. Mahakama inaendelea kusikiliza hoja za mapingamizi kisha majibu ya upande wa Jamhuri na kutoa uamuzi wa kupokea ama kukataa kupokea.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Kasekwa, Ling'wenya na Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita, likiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

## Faini mil. 1.5/- kisa nyama ya nyumbu

**Said Hamdani,** LINDI

IDARA ya wanyamapori wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, imemtoza faini ya Sh 1,500,000 mkazi wa jijini Dar es Salaam, Ally Salee Mfikilwa (43), baada ya kukamatwa akiwa anasafirisha vipande nane vya nyama ya nyumbu bila ya kuwa na kibali.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, alibainisha hayo, huku akieleza kuwa Mfikilwa alikamatwa kijiji cha Nangando,karibu na kituo cha mafuta cha Rashal Desemba 6 mwaka huu majira ya mchana.

Alisema askari wa wanyamaori wakishirikiana na jeshi la polisi wilaya ya Liwale, walimkamata Mfikilwa akiwa na vipande vinane vya nyama hiyo vyenye uzito wa kilo nane ya thamani ya dola 650 za Kimarekani (sawa na Sh.milioni 1.5 ).

Kitinkwi alisema alikuwa ameiweka ndani ya mfuko mweupe wa salfeti na kuipakia kwenye kebini ya gari aina ya Scania Namba T.719 CDC iliyokuwa na tela T.342 AMJ,akiisafirisha kutoka Wilaya ya Liwale kuelekea Dar es Salaam.

Alisema wakati Mfikilwa anakamatwa, dereva na utingo wa lori hilo ambao hata hivyo, majina yao hayajafahamika, walifanikiwa kutoroka, huku mtuhumiwa akifikishwa ofisi za wanyamapori mjini Liwale na kutakiwa kulipa Sh. milioni 1.5 na kuendelea na safari yake.

Kamanda huyo alisema Mfikilwa alilipa faini hiyo na kuendelea na safari yake ya Dar es Salaam.

Kitinkwi aliwataka wananchi wanaojihusisha na biashara haramu zilizo nje ya utaratibu wa kisheria, zikiwemo maliasili ya Taifa kuacha mara moja, badala yake wafanye kazi halali kukwepa mkono wa dola.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TANGAZO KWA UMMA

## UZINGATIAJI WA MATAKWA YA SHERIA KUHUSU KUTUNZA AKAUNTI YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wote waliosajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa upande wa Tanzania Bara, kutunza Akaunti ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT Account) kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 89 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148. Akaunti hizo zinatakiwa kuwa na taarifa zifuatazo:

- Kodi kwenye mauzo kwa kipindi/mwezi husika
- Kodi kwenye manunuzi anayostahili kujirejeshea kwa kipindi husika
- Marekebisho yoyote ya kodi yanayotakiwa au kustahili kufanyika ndani ya kipindi husika

Sambamba na akaunti za VAT, walipakodi wote waliosajiliwa na VAT wanakumbushwa kutunza kumbukumbu na taarifa zote za masuala ya VAT kama inavyotakiwa katika kifungu cha 89 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148.

Wafanyabiashara wote waliosajiliwa na VAT wanakumbushwa kuzingatia matakwa haya ya kisheria ili kuepuka madhara au adhabu na hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji biashara na usumbufu usio wa lazima.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea ofisi yoyote ya TRA iliyokaribu na wewe au wasiliana nasi kupitia barua pepe na namba za simu kama ifuatavyo:

***Namba za Bure*** : 0800 750 075
0800 780 078

***WhatsApp:*** 0744 23 33 33

***Barua pepe :*** huduma@tra.go.tz
services@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

***Imetolewa na;***
**KAMISHNA MKUU**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siasa safi muhimu

**JANA** vyama vya siasa kupitia baraza lao vilikutana kujadili demokrasia nchini msisitizo ukiwa ni namna gani ya kufanya siasa za kistaarabu zenye kutoa usawa kwa wadau wote pamoja na kufuta yaliyotokea nyuma yaliyojeruhi mioyo ya wengi.

Akiufungua mkutano huo jijini Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kikao hicho kijadili na kuja na mapendekezo ya namna ya kufanya mikutano ya hadhara pasipo kujeruhi, maneno makali, kufanya vurugu na kuharibu utulivu na amani ya nchi.

Hata hivyo, CHADEMA na NCCR-Mageuzi havikushiriki kwa kile vilichokieleza ni mambo ya msingi viliyoyataka serikali iyafanyie kazi ikiwamo kufutiwa kesi Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Kuwepo kwa kikao hicho ni muhimu katika kutibu majeraha ya uchaguzi wa mwaka 2020 ambao ulisababisha baadhi ya watu kuwa na chuki na majeraha mioyoni mwa mengi yanayoelezwa kuwa yalisababishwa na uchaguzi huo ambao hata baadhi ya viongozi wakuu wastaafu wanasema ulitawaliwa na kasoro nyingi.

Tunaamini kuwapo kwa mkutano huo ni kujenga msingi wa siasa za kistaarabu ili kuepusha maumivu ambayo siyo ya lazima kwa kuwa siasa siyo vita, chuki, maumivu na kushambuliana kimwili na kwa maneno.

Pia, Jeshi la Polisi lilijikuta kwenye lawama ambazo ni endelevu kwa kuwa kila baadhi ya vyama vinapoomba kibali cha kufanya mikutano dakika za mwisho linatolewa zuio kuwa kuna taarifa za kiitelejensia ambazo zimeonyesha kutakuwa na uvunjifu wa amani, jambo ambalo limewafanya wadau wengine wa siasa kujiona wanyonge kwenye siasa za nchi.

Ni lazima kukomesha siasa za chuki na uhasama, ambazo kwa kiasi kikubwa zitakwamisha maendeleo, na mara kadhaa imejitokeza kwa mamia kujiandikisha kupiga kura, lakini hawajitokezi kwa wingi kupiga kura kutokana na mazingira ambayo hutengenezwa wakati wa mchakato wa uchaguzi.

Jana Rais Samia alisema ni vyema ikaeleweka kuwa siasa siyo kulumbana, siyo matusi, kusema uongo na kwamba kuna usemi ukitaka kusema uongo nenda kwa wanasiasa, lakini siyo kweli kwa kuwa siasa siyo kusema uongo, lugha za dhihaka, maneno ya kashfa au kuchochea watu wasishiriki shughuli za maendeleo na kutotii sheria.

Alisema siasa siyo uchonganishi kati ya wananchi na serikali yao, na kwamba siasa za muundo huo hazina tija bali ni ukikwaji wa kanuni za demokrasia na ushindani.

Tunampongeza Rais Samia kuonyesha nia na utashi wa kujenga siasa za kistaarabu, uwanja sawa pamoja na kuvumiliana hususani kauli yake kwamba Watanzania tufungue ukurasa mpya kwa kuweka kando mambo yaliyopita pamoja na kutamka kwamba yupo tayari kusamehe na kuwa tayari kukosolewa.


Tunaamini siasa safi itatoa motisha kwa wananchi kushiriki maendeleo na kuwa na imani ya wanaowachagua, lakini Jeshi la Polisi lisikubali kutekeleza majukumu yake kwa kuvinyima haki baadhi ya vyama vya siasa.

Kuwapo kwa mazungumzo baina ya wadau wote wasiasa ni muhimu, na zaidi lazima kuwaleta pamoja walioshindwa kushiriki mkutano huo kwa sababu ambazo wanaziona ni za msingi ili kujenga umoja wa kitaifa, mshikamano na maridhiano pasipo kumuacha yeyote kando.

Tanzania ni ya wote kama alivyoeleza Rais Samia kuwa hakuna mwenye hati miliki na itajengwa kwa ushirikiano wa wote, lazima ilindwe kwa wivu mkubwa na viashiria vyovyote vya uvujifu wa amani visiangalie itikadi ya chama, rangi, eneo analotoka mtu, cheo au kazi yake.

Tunaamini mkutano huu utatoka na mapendekezo mengi na yenye tija ambayo yatakuwa suluhisho la migogoro ya kisiasa iliyokuwepo nchini, kiasi cha baadhi ya viongozi wa dini kuomba wakuu wa nchi kutibu majeraha na makovu ya mioyo ya wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wewe ni fundi viatu? Soma orodha hii ya kazini kwako, isikuangamize kiafya

Na Sabato Kasika

**MAFUNDI** wengi wa viatu wana kawaida ya kufanya kazi yao bila kuchukua tahadhari za kiafya, hali ambayo inaweza kusababisha wakaambukizwa magonjwa mbalimbali bila wao kujua.

Imebainika kuwa wanapofanya kazi hiyo ya kushona viatu, huwa hawachukui tahadhari kwa kuvaa 'glovusi', hali inayoweza kuwaweka katika hatari ya kupata fangasi, tetenasi, ukoma na hata wakati mwingine Ukimwi.

Hiyo inatokana na kwamba, wakati mwingine wateja wanaweza kuwa na fangasi au ukoma, ambazo zikiwa na majimaji na kisha fundi akayagusa huku akiwa na michubuko, inakuwa rahisi kuambukizwa magonjwa hayo.

Pia inaelezwa kuwa viatu vinaweza kuwa na vipande vya misumari ndani vyenye kutu, na kwamba ikiwachoma ni rahisi kupata ugonjwa wa tetenasi na hivyo kuweka afya katika hatari.

Mafundi hao pia wanakuwa katika hatari ya kupata ugonjwa wa Ukimwi kupitia majimaji ambayo yatakuwa ndani ya viatu, hasa wanapokuwa na michubuko kwenye vidole vyao na kugusa majimaji hayo.

Dk. Phoibe Koshuma, mtaalamu wa magonjwa ya ngozi mstaafu wa Kituo cha Afya Sinza, Dar es Salaam, anasema mafundi wengi wanaoshona viatu, hawachukui tahadhari katika kazi yao hiyo.

Kwamba, wanakinga nguo zao zisipate uchafu badala ya kujikinga na magonjwa hayo kwa kuvaa 'glovsi', ili kuwa salama zaidi dhidi ya magonjwa ya ngozi na mengine yanayoweza kuhatarisha maisha yao.

Mtaalamu huyo anashauri mafundi wawe makini kwa kutumia glovusi wanapofanya kazi zao za kushona viatu, kwamba badala ya kulinda zaidi nguo zao zisichafuke, walinde afya zao kwanza.

Katika ufafanuzi wake, anaweka wazi kuwa katika maduka ya vifaa vya ujenzi, kuna 'glovusi' za plastiki na ngozi laini ziitwazo 'heavy duty', kwamba wakizivaa wanakuwa salama zaidi kuliko kufanya kazi hiyo kwa mazoea.

Dk. Koshuma anafafanua kuwa mbali na hizo, zipo 'glovusi' nyingine za vitambaa ambazo ndani yake zina nailoni, ili kuzuia majimaji kupenya na kwamba, ni muhimu wajali afya zao kwa kutumia vifaa hivyo.

Kwa maelezo hayo ya mtaalamu wa afya, ni wazi kwamba kuna haja mafundi viatu kuwa makini kwa kuchukua hatua zinazoshauriwa, kwa ajili ya usalama wa afya zao, huku wakiendelea kuhudumia wateja wao.

Ninakubaliana na mtaalamu huyo kwamba ni kweli mafundi wengi huweka vitambaa juu ya miguu, ili kuzuia uchafu wa viatu usiguse nguo zao, lakini kwenye suala la kuvaa 'glovsi' hawana habari nalo.

Hivyo kwa ushauri huo wa bure, ingekuwa ni vyema kama kila fundi viatu atachukua hatua sahihi zinazotakiwa, kwa ajili ya kulinda afya yake kuliko kuendelea kufanya kazi hiyo kwa mazoea ya siku zote.

Ikumbukwe dunia imebadilika, magonjwa yameongezeka, hivyo kwa mazingira wanayofanyia kazi, ni wazi kwamba bila kubadilika, inakuwa ni rahisi kukumbwa na mojawapo ya magonjwa yaliyotajwa na mtaalamu wa afya.

Ni vyema kila fundi viatu akatambua kuwa mtindo aliozoea wa kushona viatu bila tahadhari, anaweka rehani afya yake kwa kutojua au kwa kujua, hivyo jambo la msingi ni kutafakari na kuchukua hatua zinazoshauriwa.

**Katika ufafanuzi wake, anaweka wazi kuwa katika maduka ya vifaa vya ujenzi, kuna 'glovusi' za plastiki na ngozi laini ziitwazo 'heavy duty', kwamba wakizivaa wanakuwa salama zaidi kuliko kufanya kazi hiyo kwa mazoea.**

HABARI KITAIFA

# Serikali yasisitiza uwekezaji mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

SERIKALI itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano ili itoe mchango mkubwa zaidi katika kuchochea shughuli za maendeleo.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alibainisha hayo jana alipozindua mnara wa mawasiliano katika kijiji cha Kasumo, kata ya Kajana wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma.

Alisema mnara huo ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana nchi nzima na kwa gharama nafuu ili kuwawezesha wananchi wanaoishi pembezoni na hasa vijijini, kumudu matumizi ya huduma hiyo.

Alisema ujenzi wa mnara katika kijiji cha Kasumo ni mwendelezo wa jitihada za serikali kuufungua mkoa wa Kigoma na kuwezesha wananchi kutumia huduma za intaneti, ambazo pia zitaboresha huduma za kijamii na kufungua fursa za kiuchumi.

Dk. Mpango aliwaeleza wananchi fursa zitakazopatikana kutokana na matumizi ya intaneti na mawasiliano ya simu kwa ujumla ni pamoja na kuwaunganisha wananchi wa kata ya Kajana, kata ya Muyamba na vijiji jirani, pia kuunganishwa na masoko ya mazao yanayozalishwa katika wilaya hiyo na biashara mbalimbali zinazofanyika katika wilaya hiyo.

"Mtandao wa simu unatuwezesha kuongeza na kupanua mtandao wa wateja na hivyo kurahisisha shughuli mbalimbali za kiuchumi," alisema Dk. Mpango.

Alibainisha kuwa kupitia mnara huo, wananchi watawasiliana moja kwa moja na vyombo vinavyotoa huduma muhimu za kijamii pamoja na kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wa kilimo, ufugaji na kuboresha shughuli zao, huku wanafunzi wa shule za msingi hadi vyuo wakinufaika kwa matumizi ya intaneti kujisomea na kujipatia maarifa mapya.

Kwa kuzingatia faida na fursa zinazopatikana katika huduma ya mawasiliano, Dk. Mpango aliwataka wananchi wa kijiji cha Kasumo na wilaya nzima ya Buhigwe kulinda na kutunza miundombinu hiyo kwa kuwa imegharimu fedha nyingi za serikali.

Alisema uharibifu wa miundombinu hiyo utaleta hasara na madhara makubwa kwa wananchi wa Buhigwe na Kasulu kiuchumi na kijamii.

"Ukiharibiwa huu mtambo maana yake tutakosa huduma ya mawasiliano pamoja na faida zote za huduma hii zitapotea na hivyo kurudisha nyuma juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo," alisema .

Dk. Mpango pia aliwataka wananchi hao kutumia vyema huduma hiyo na kujiepusha na matumizi mabaya ya mitandao ikiwamo kutazama na kusambaza picha ambazo hazina maadili kulingana na tamaduni za kitanzania.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, alilipongeza Shirika la Mawasiliano (TTCL) kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kufikisha huduma ya mawasiliano ya uhakika kwa wakazi wanaoishi katika kijiji cha Kasumo pamoja na vijiji jirani.

Alisema mnara huo utatoa huduma ya intaneti kwa kasi ya 4G ambayo imekuwa ni hitaji msingi kwa maisha ya mwanadamu katika dunia ya sasa na kwamba mnara huo unaenda kufanikisha ajenda ya serikali ya kufikisha huduma ya intaneti hadi ngazi ya vijiji.

Akisoma taarifa ya mradi wa mnara huo Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, alisema mradi huo umekamilika katika kipindi cha miezi miwili, ukigharimu Sh. 326,874,773.75 (mil 326.875).

Kindamba alisema TTCL imetoa Sh. 208,624,772.75 huku serikali kupitia UCSAF ikitoa Sh. 118,250,000.

Mkurugenzi Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, alisema jukumu kubwa la taasisi yake ni kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini na mipakani mwa nchi wanapata huduma za mawasiliano.

# Diaspora wabainisha mikakati kuinua uchumi

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Tanzania Diaspora Hub (TDH) inayojihusisha na uwekezaji, imebainisha mikakati mitatu inayolenga kuinua uchumi wa taifa sambamba na kutia saini mkataba wa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa TDH, Nassor Basalama, alisema mikakati hiyo ni pamoja na kuitikia wito wa Rais Samia Suluhu Hassan katika kufanya uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mkakati mwingine ni kupanua soko la kimataifa kwa wafanyabiashara na kushawishi wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali kuja kuwekeza, huku akibainisha kuwa umoja wao ni kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja katika maeneo tofauti nchini.

"Kaulimbiu ya TDH ya Wekeza Nyumbani, ilianzishwa nchini Marekani na imewaunganisha zaidi ya wawekezaji 180 kutoka nchi 18. Katika hatua za awali tunatarajia kuzindua miradi mitatu nchini ambayo tayari utekelezaji wake ulishaanza.

"Miradi hiyo ni pamoja na uwekezaji wa samaki uliopo wilayani Korogwe, mradi wa katani mkoani Tanga na mradi wa kilimo cha parachichi ambazo zitatumika kutengeneza bidhaa mbalimbali zitakazosaidia kutoa fursa za ajira lakini pia kuinua pato la taifa," alisema Basalama.

Katika kuunga mkono jitihada za serikali kuinua uchumi wa taifa, alisema fedha zote walizozikusanya kwa ajili ya kuingia katika miradi zimehifadhiwa katika benki za Tanzania, jambo ambalo limeweza kunufaisha taasisi hizo nchini.

Pia alisema sehemu kubwa ya wanaoshirikiana nao katika uwekezaji ni wilaya, hivyo alitoa wito kwa wakuu wa wilaya kuwapa ushirikiano ili kurahisisha jitihada zao, huku akisisitiza kuwapo kwa mipango mkakati itakayoweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili isaidie kuongeza tija katika uwekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Francis Nanai, alisema ndani ya taasisi hiyo sera yao kubwa ni kuwa shirikishi, kuhakikisha kila mwekezaji na mfanyabiashara wa ndani na nje ya nchi anayependa kuwekeza nchini wanamsaidia ili kutimiza malengo ya kufanya uwekezaji.

Pia alisema ndani ya TPSF wana sekta 14 lakini katika mwaka huu wamechukua wajumbe kutoka TDH ili kuongeza nguvu hasa katika kushauriana na kuona namna bora ya kufanya uwekezaji zaidi na wenye tija nchini.

"Suala la diaspora ndani ya TPSF ni ajenda kubwa kwa sababu tunajua kwamba wanaweza kuwa wawekezaji wakubwa hata kupita mwekezaji mmoja mmoja ambao tunawakimbilia kutoka nchi za nje. Wao ni Watanzania, hivyo wanawiwa kuona kuwa nchi yao inafanikiwa katika maendeleo ya kiuchumi na kibiashara.

"Pia fedha ambazo watakuwa wamezipata katika juhudi zao za kujiendeleza katika masuala mbalimbali ya kiuchumi kule waliko wangependa kuona zinatoa manufaa makubwa ndani ya nchi yao, hivyo tunaona ni chanzo kizuri cha kutuongezea uelewa na ujuzi ambao tukiutumia tunaweza kupiga hatua kwa haraka," alisema Nanai.

Alibainisha kuwa TDH wana weledi wa ufanyaji kazi pamoja na uwezo wa mitaji, hivyo kutoa wito kwa serikali kuwa na diplomasia nzuri ya uchumi itakayowavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini ili kuinua zaidi pato la taifa.

INSURANCE GROUP OF TANZANIA LIMITED
12TH FLOOR, NIC INVESTMENT HOUSE, SAMORA AVENUE, DAR ES SALAAM
Tel: +255 22 2131481/ +255 22 2122064, Fax: +255 22 2131482,
E-mail: info@igt.co.tz, Website: www.igt.co.tz
P.O. Box 665, Dar es Salaam
always with you

TANGAZO



Mr. Thompson Onesmo Mwanri

**Insurance Group of Tanzania Limited** ingependa kuufahamisha umma kuwa **Mr. Thompson Onesmo Mwanri** siyo muajiriwa wa kampuni hiyo ya **Insurance Group of Tanzania Limited** kuanzia tarehe **15 December 2021**.

Hivyo, **Insurance Group of Tanzania Limited** haitohusika wala kuwajibika kwa makubaliano yoyote yale yatakayoingiwa naye kwa jina la kampuni ya **Insurance Group of Tanzania Limited** kupitia yeye.

**Menejimenti ya IGT.**

TANGAZO



Mr. Francis Paul Pamba

**Insurance Group of Tanzania Limited** ingependa kuufahamisha umma kuwa **Mr. Francis Paul Pamba** siyo muajiriwa wa kampuni hiyo ya **Insurance Group of Tanzania Limited** kuanzia tarehe **29 November 2021**.

Hivyo, **Insurance Group of Tanzania Limited** haitohusika wala kuwajibika kwa makubaliano yoyote yale yatakayoingiwa naye kwa jina la kampuni ya **Insurance Group of Tanzania Limited** kupitia yeye.

**Menejimenti ya IGT.**

# Waziri atema cheche ujenzi Kigongo- Busisi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amemwagiza mkandarasi na msimamizi wa mradi wa ujenzi wa daraja la JPM lililounganisha eneo la Kigongo-Busisi kuhakikisha linajengwa kwa viwango vinavyostahili.

Akikagua maendeleo ya daraja hilo lenye urefu wa kilometa 3.2 linalojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 716.33, alisema hataki kujengewa daraja la kubabaisha bali la kiwango kinachotakiwa kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.

Mbarawa aliagiza kazi hiyo kufanyika usiku na mchana ili ikamilike kwa wakati na serikali haitaki kazi za kubahatisha na kubabaisha.

Aliongeza kuwa daraja hilo linalojengwa na serikali, limeandika historia na ujenzi huo unaotumia teknolojia ya kisasa unatokea mara moja na kuomba litumike kama shule ya kuwafundisha Watanzania jinsi ya kutengeneza madaraja.

"Nimeambiwa kuna vijana 11 nataka kuona vijana wetu kama 21 wanafanya kazi hapa kama kuwalipa 300,000 kwa mwezi si tatizo kwani hatushindwi kwa sababu tunajenga miradi hii ya kimkakati. Ninaagiza Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoani Mwanza, tunataka vijana waje kujifunza kwa sababu fursa hii haitopatikana tena.

Tunataka daraja ili lizalishe wahandisi 11 wa madaraja tunaamini tukiweka mikakati vizuri tutatoa vijana wazuri," alieleza Waziri.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mwanza, Boniface Mkumbo, alisema mradi huo umefikia zaidi ya asilimia 34 ingawa kazi inaonekana iko chini kwa asilimia 16 na kwamba wamejipanga kufidia kwa kuongeza wafanyakazi 720 kutoka 461 waliokuwapo awali.

Alisema vifaa vimeongezwa na watakwenda kama mpango kazi unavyoonyesha na kuahidi kutekeleza maelekezo ya waziri ili kwenda na wakati na kuhakikisha kazi inakwenda kwa viwango kama ilivyosanifiwa na kuisha kwa wakati uliopangwa.



Kiongozi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Benki ya NMB, Agness Shawa (kulia), akifafanua jambo kwa baadhi ya wanafunzi kutoka shule tofauti za msingi na sekondari walio katika programu ya 'Children Boot Camp', kuhusu kupanda na kushuka kwa thamani ya fedha za kigeni, wakati walipofanya ziara ya kimasomo katika Makao Makuu ya Benki hiyo, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi madarasa Iringa watia fora

**Na Steven William,** IRINGA

WILAYA ya Iringa inatarajia kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 66 katika shule za sekondari zikiwamo shule shikizi 28 ili kutoa nafasi kwa wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza mwezi ujao.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, aliyasema hayo juzi baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari katika wilaya hiyo.

Alisema katika Wilaya ya Iringa, wanajenga vyumba vya madarasa katika shule za sekondari na kwamba katika baadhi ya shule, ujenzi umefikia hatua za mwisho kwa kuweka madirisha ya vioo.

Kwa mujibu wa Moyo, wakati wowote kuanzia sasa, mafundi watakabidhi vyumba hivyo vya madarasa kwa kuwa ujenzi umefikia hatua za mwisho baadhi ya sekondari na shule shikizi.

Alisema kwa kushirikiana na viongozi wa chama na serikali pamoja na kamati ya ulinzi na usalama wamesimamia ujenzi huo huku wananchi pia wakichangia nguvu kazi.

Moyo juzi alikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule zasekondari za Nyerere, Nyang'oro, Furahia, Kiwale, Ilambilole, Isimani na zile za shikizi ambazo ni Kibaoni, Kigasi, Ikengeza ambazo ziko hatua ya umaliziaji ujenzi wake kwa kuweka vigae.

# Serikali yatoa mwongozo kwa madalali

**Na Munir Shemweta,** WANMM

SERIKALI imetoa muongozo wa kusimamia shughuli za udalali nchini kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zitakazoleta tija kwa serikali na jamii kwa ujumla.

Mwongozo huo una madhumuni ya kutambua madalali, shughuli zao, mahali wanapofanyia kazi, utaratibu wa kuratibu na kudhibiti shughuli za udalali pamoja na kulinda maslahi ya wateja, wamiliki, madalali na serikali.

Walengwa wa mwongozo huo ni madalali wa nyumba, majengo, viwanja na mashamba, serikali kuu na serikali za mitaa, sekta binafsi, wananchi na wadau wote katika shughuli za udalali wa nyumba, majengo, viwanja na mashamba.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi alipokutana na wawakilishi wa kampuni za uuzaji na upangishaji nyumba, viwanja na mashamba pamoja na madalali mmoja mmoja.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, mwongozo huo unamtaka kila dalali anayepangisha, kuuza kiwanja au kupangisha nyumba kusajiliwa na usajili huo utafanyika kuanzia Januari, mwakani.

Alizitaja sifa na vigezo ambazo madalali watatambulika kupitia mwongozo huo kuwa ni pamoja na kuwa raia wa Tanzania mwenye akili timamu na umri usiopungua miaka 18, anwani au namba ya simu au utambulisho kwa mfumo wa kieletroniki (barua pepe), mahali pa kufanyia kazi panapofahamika, kuwa na namba ya mlipakodi, kitambulisho cha taifa na kuwa na cheti cha utambulisho kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

"Kupitia mwongozo huo, utambuzi wa madalali utafanywa na idara mpya ya mipango miji na mazingira katika miji na katika halmashauri za wilaya," alisema Lukuvi.

Alisema baada ya taratibu kukamilika, halmashauri husika itampa mwombaji utambulisho wa kufanya shughuli za udalali wa nyumba, majengo, viwanja na mashamba na kusisitiza mtu au kampuni yoyote itatakiwa kufuata taratibu ikiwamo kujaza fomu ya maombi ya usajili, kuwasilisha barua ya utambulisho kutoka serikali za mitaa na kulipa ada ya utambulisho Sh. 20,000 kwa kila mwaka.

Waziri Lukuvi alisema katika mwongozo huo, kuna makatazo ambayo dalali hatakiwi kufanya kwenye shughuli zake na kuainisha baadhi kuwa ni pamoja na kufanya kazi bila kutambuliwa na halmashauri, kukwepa kodi, kufanya udanganyifu, kupokea malipo tofauti na malipo yaliyotajwa na kushawishi au kushinikiza mmiliki kutoza au kulipa bei tofauti na makubaliano.

Waziri Lukuvi aliwataka madalali waliohudhuria mkutano huo kufanya kazi kwa maadili kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakifanya kazi kwa lengo la kujipatia kipato kikubwa na kudhulumu wananchi huku wakishindwa kuchangia kodi na mapato ya serikali.

Naye Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula aliwataka madalali kutafakari na kuyafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na serikali na kusisitiza kuwa lengo la serikali ni kuona madalali wanafanya kazi zao bila kubughudhiwa lakini kwa kufuata sheria na taratibu.

"Niwaombe madalali mtafakari maelekezo ya serikali maana lengo ni kuona mnafanya kazi zenu bila kubughudhiwa" alisema.

Baadhi ya madalali waliishukuru serikali na kuwapatia mwongozi ambao sasa utatambua kazi wanazofanya huku wakiiomba serikali kuweka mfumo rahisi utakaowawezesha kulipa kodi.

# Madini ya graphite yatakavyoleta neema

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa kampuni ya uchimbaji madini ya Black Rock, kutoka Australia, John de Vries, amesema Tanzania inatarajia kupata maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii kupitia madini ya graphite (kinywe) yatakayochimbwa katika mgodi wa Mahenge Ghaphite, mkoani Morogoro.

Vries aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya utiaji saini mikataba kati ya serikali na kampuni za uchimbaji madini ikiwamo ya Black Rock ambao ulishuhudiwa Jumatatu na Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo alisema mgodi wa Mahenge ambao utakuwa unafanya shughuli za uchimbaji wa madini hayo Mahenge kupitia ubia na Kampuni ya Faru Corporation, wakati wote wa uhai wake faida ya jumla kwa uchumi wa Tanzania itakuwa Dola za Marekani bilioni 6.5 (sawa na Sh. trilioni 15).

Serikali ina miliki asilimia 16 ya hisa za riba na zisizo na malipo Faru na asilimia 84 ikimilikiwa na Black Rock kupitia Kampuni zake tanzu ya Uingereza, Mahenge Resources.

Vries aliishukuru serikali chini ya Rais Samia kwa imani ambayo imeweka katika kuthibitisha ushirikiano wa muda mrefu na Black Rock ili kuendeleza kwa pamoja mgodi huo.

"Tumetiwa moyo sana na mazingira mapya ya uwekezaji yaliyopo sasa Tanzania. Chini ya makubaliano haya Tanzania itakuza uchumi wake kupitia makusanyo ya ushuru, kodi na gawio.

Alitaja manufaa mengine kuwa ni mgodi huo utatoa ajira 970, ununuzi wa bidhaa na huduma, upatikanaji wa nishati, usafirishaji kupitia reli na Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kusainiwa kwa makubaliano hayo kumeweka mazingira ya kuanza utekelezaji wa mradi huo ambao utakuwa na manufaa kwa wananchi wa Wilaya ya Ulanga, Mahenge na hatimaye uchumi wa nchi kukua.

Mwezi Aprili 2018, wananchi wa Mahenge walishuhudia tani 500 zikisafirishwa kupitia usafiri wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA), katika stesheni iliyopo Ifakara kuelekea Bandari ya Dar es Salaam kuzisafirisha kwenda Canada.

Februari mwaka 2020, kampuni ya Mahenge iliwakabidhi wanavijiji wa Mdindo, Kisewe na Nawenge wilayani Ulanga, majengo matatu mapya ya ofisi za vijiji.

Madini ya Kinywe yanatumika kutengeneza bidhaa mbalimbali, kama breki, kinga za mashine, betri za simu, kompyuta mpakato (Laptop) na penseli.

Mikoa ambayo imegundulika kuwa na madini hayo ni pamoja na Morogoro, Lindi, Mtwara, Manyara na Tanga.

Uwepo wa Kinywe, unaifanya Tanzania kuwa moja ya mataifa yanayozalisha kwa wingi madini hayo ambapo kupitia miradi mitatu mikubwa ina uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 240,000 kwa mwaka na utaifanya kuwa nchi ya pili kwa uzalishaji wa madini hayo duniani ikitanguliwa na China inayozalisha zaidi ya tani 700,000.

India inashika nafasi ya tatu kwa kuzalisha tani 170,000 na Brazil nafasi ya nne ikizalisha tani 800,000, Canada, Korea Kusini na Uturuki wanazalisha tani 30,000. Zingine ni Russia inayozalisha tani 14,000, Mexico tani 8,000, Ukraine na Zimbabwe tani 6,000, Madagascar tani 5,000, Sri Lanka tani 4,000, Norway tani 2,000 na nchi nyingine zinazalisha tani 1,000.




Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Usambazaji Vodacom Tanzania PLC, George Lugata (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa kutangaza ofa mpya ya "Pata simu Lipa kidogo kidogo" ambapo wateja wa Vodacom wataweza kununua simu janja aina ya Samsung kwa kulipia shilingi 80,000 na kuendelea kulipia kwa muda wa siku 300. Kushoto ni Mkurugenzi wa d.light Tanzania, Charles Natai, ambao ni washirika wa ofa hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tigo na Infinix sasa waja na simu ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya utoaji wa huduma za kidigitali ya Tigo Tanzania, imeshirikiana na INFINIX Tanzania kuzindua simu ya INFINIX Hot 11 Play.

Kampuni hiyo imesema itauza kwa rejareja kwa shilingi 360,000 na HOT 11 kwa shilingi 405,000

ushirikiano kati ya INFINIX na Tigo huwapa wateja zaidi – huku simu mahiri ya kisasa ikija na intaneti ya 78GB kutoka TIGO bila malipo kwa mwaka mzima.

Meneja Biashara wa Tigo, Seleiman Bushagama akizungumza wakati wa uzinduzi huo, alisema: "Ushirikiano wetu na INFINIX ni jambo la kujivunia kwa sababu unaendana vyema na maono yetu ya kusambaza ulimwengu mpya wa kidijitali kwa wateja. Uzinduzi huu wa aina nyingine ya juu zaidi, simu mahiri ya bei nafuu, ni uthibitisho wa dhamira yetu ya kuhakikisha kwamba kila mtu anafurahia manufaa ya maisha ya kisasa yaliyounganishwa kupitia huduma na bidhaa tunazotoa."

Bushagama alisema washirika wao wanaendelea kuamini chaneli zao za usambazaji, mtandao mpana wa 4G, na kwamba unalenga kuongeza kasi ya kupenya kwa simu mahiri nchini huku wakihakikisha kuwa wateja wanafurahia matumizi bora ya kidijitali kupitia mtandao wa kasi zaidi wa 4G+ ambao ni mkubwa zaidi nchini.

Mtandao huo unamwezesha ambapo mteja atakayenunua simu hizo kutoka kwenye maduka ya TIGO na INFINIX atapata data ya kuperuzi mitandaoni ya GB 78 bila malipo kwa mwaka mzima.

Ofisa Uhusiano wa Umma wa Infinix, Aisha Karupa alisema: "Tulibuni HOT 11 play na HOT 11 tukizingatia uzoefu wa mtumiaji kwa kuipa simu betri yenye uwezo wa kudumu na chaji muda mrefu ya 6000mAh yenye chipset ya G37 kwa ajili ya utendaji wa kiwango cha juu kwa wale wapenzi wa GAMES pamoja na 6.82 silky. Kioo laini chenye kiwango cha FHD+ na 90Hz ambacho kitamwezesha mtumiaji kutazama picha na video kwa ubora ule ule."

# Wadau wafurahia mradi wa HakiElimu kuwabakiza shuleni

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Vigh`awe iliyoko wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma wamesema mradi wa kupunguza mdondoko wa elimu kwa wanafunzi (GRTI), umewasaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa changamoto walizokuwa wakikumbana nazo awali.

Mradi huo wa kusaidia wanafunzi kubaki shuleni ulianzishwa na Taasisi ya HakiElimu mwaka jana kwa ajili ya kusaidia kupunguza baadhi ya changamoto za wanafunzi kwenye shule mbalimbali na miongoni mwa shughuli zake ni kutoa elimu ya kujitegemea kwa wanafunzi shuleni na kuwafundisha kujiamini.

Pia, unasaidia kutoa taulo za kike kwa wasichana shuleni na vifaa vya wanafunzi kujifunzia ujasiriamali ikiwamo mashine za kushonea nguo.

Anna Songoro, mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, alisema tangu kupelekwa kwa mradi huo shuleni kwao, hawatoroki tena.

"Pamoja na kutusaidia yote ambayo tumesaidiwa ikiwamo mashine za kushonea nguo, lakini kubwa zaidi ambalo tumelifurahia ni kutuletea taulo shuleni, tumekuwa tukihangaika sana kabla ya hapo, unapoingia kipindi cha hedhi ilikuwa inatubidi tutoroke kwa kukosa vya kujisitiri na kuogopa kuaibika, hata ukilazimisha kubaki shuleni huwezi kuwa na amani, huwezi kujiamini,"alisema Anna.

"Lakini kwa sasa hakuna anayeondoka hata ukiwa kwenye hiyo hali, huwa tunakwenda kuchukua kwenye ofisi ya mwalimu, unajisitiri na unaendelea na masomo kama kawaida, hili limetusaidia sana na tunasoma kwa uhuru zaidi."

Jambo jingine alisema kupitia mradi huo, pia wanafundishwa elimu ya kujitambua na kutambua haki zao za msingi.

Irene Masinga, naye ni mwanafunzi wa kidato cha nne shuleni hapo, alisema elimu ya kujitambua ambayo wamepatiwa kupitia mradi huo, imewasaidia kuwafumbua macho na kwamba na wao kwa sasa wamekuwa mabalozi wa kuwafundisha wenzao mtaani na katika shule nyingine ambazo mradi huo haujafika.

"Sasa hivi tumejiamini sana, akili imefunguka na tunapita mitaani kuwaelimisha wasichana wenzetu namna ya kujitambua, kujua haki zetu za msingi na namna ya kupambana na vitendo hatarishi kwenye maisha yetu,"alisema Irene.

Mkuu wa Shule hiyo, Elias Daudi, alisema mradi huo umepunguza vitendo vya utoro kwa kiwango kikubwa shuleni hapo tofauti na ilivyokuwa awali na kuongeza ufaulu.

"Kwa sasa watoto wengi tunaona wanabaki shuleni muda wote, kabla ya hapo kulikuwa na utoro mwingi sana hasa kwa watoto wa kike, walikuwa wanasumbua sana kipindi cha nyuma kabla ya kufika mradi huu wa kuwapatia taulo za kike," alisema Daudi.

"Na hata hii elimu ya kujitambua ambayo wanafundishwa kwa sasa umewafungua sana, na huu ni mwaka mmoja tu tangu uanzishwe na HakiElimu, tunaamini kwamba kadri siku zinavyokwenda utakuwa na matunda mazuri zaidi."

# Wataka kasi mabadiliko Sheria ya Ndoa

Na Zuwena Shame

WADAU wa masuala ya haki za mtoto wa kike nchini wameiomba serikali kuharakisha utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa nchini kwani ucheleweshwaji wake unaweza kuongeza idadi ya ndoa za utotoni.

Mahakama Kuu mwaka jana ilisimamia hukumu ya awali ya vifungu vya Sheria ya Ndoa vinapingana na Katiba kwa kuweka umri tofauti wa kuoa au kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Mahakama Kuu pia ilikazia kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 baadhi ya vifungu vyake vinapingana na Katiba kwa kuweka umri tofauti wa kuoa au kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume, hivyo kuitaka serikali kubadili sheria hiyo ambayo ni baguzi kwa watoto wa kike ndani ya mwaka mmoja.

Wadau hao walitoa ombi hilo jijini Dar es Salaam wakati wa mjadala uliofanyika kwa njia ya mtandao, kujadili jinsi gani janga la corona nchini limechangia wimbi la ndoa za utotoni na nini cha kufanya ili kupunguza wimbi hilo.

Mkuu wa Programu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Joyce Mkina, alisema kuwa mchakato wa mabadiliko ya sheria ya ndoa hasa kipengele cha umri sahihi wa mtoto wa kike kufunga ndoa, inaweza kuchangia ndoa za utoni kuendelea iwapo mchakato huo utachelewa.

Mkina alisema kuwa tangu Mahakama Kuu ikubali maombi hayo, utekelezwaji na mchakato wa sheria hiyo bado unasuasua, hivyo kuna hatari ya ndoa hizo kuendelea na kuleta athari katika kukwamisha mtoto wa kike kielimu.

Mkina alisema sheria hiyo itakapobadilishwa na kuanza kutekelezwa, watakaobainika kuikiuka na kupewa adhabu kali, ndoa za utotoni zitapungua kama sio kuisha kabisa.

"Katika kipindi cha janga la corona ndoa za utotoni zimeongezeka mara dufu hasa vijijini, na hii yote ni kutokana na sheria kukinzana, kwani bado inahalalisha umri wa mtoto wa kike ni miaka 15 ambapo wengi wao ni wanafunzi," alisema Mkina.

Alisema pia kilisababisha mimba za utotoni kwa kuwa watoto wa kike hawakuwa na ulinzi kutokana na wengi kuwa na vishawishi mbalimbali wakiwa majumbani.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Hope for Girls and Women in Tanzania, Robhi Samwelly, alisema kipindi cha likizo ya corona taasisi hiyo iliwaokoa watoto wa kike walikokuwa wanatarajiwa kuketwa na kuozwa, hivyo kuwapa hifadhi katika nyumba salama.

Alisema kuwa sheria ya ndoa itakuwa chachu ya kukomesha ndoa za utotoni iwapo mzazi au mlezi akibainika kuikiuka. Naye mwanasheria Rachel Magege kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), alisema Sheria ya Ndoa 1971 bado inaipa uhalali umri wa miaka 15 kuwa sahihi kwa mtoto wa kike kuolewa, lakini bado mtoto anakuwa bado hajui majukumu ya ndoa, hivyo kumkatisha ndoto zake kielimu. Magege alishauri pia ni vyema waathirika wa ndoa hizi kujitokeza na kuelezea vikwazo walivyopitia kama njia mojawapo itakayosaidia uharaka wa mchakato wa mabadiliko ya sheria ya ndoa. Mbunge wa Viti Maalum, ambaye alikuwa mgeni rasmi, Najma Giga, alisema ili kurahisisha mchakato wa sheria ya ndoa, wadau zikiwamo taasisi zisizo za serikali ni muhimu kufanya kazi kwa ukaribu zaidi na serikali ili kuharakisha mabadiliko ya sheria hii.

Giga alisema pia takwimu za ndoa za utotoni zimekuwa changamoto kwa sababu ndoa hizo kuwa hazisajiliwa kisheria na zimekuwa zikifanyika kwa usiri kwani watekelezaji wake wanakwepa mkono wa sheria.

Giga aliongeza kuwa Tanzania imeshindwa kusaini mkataba wa sheria ya jinsia kwa nchi za SADC ambao kipengele mojawapo ni ulazima wa kutumia njia za uzazi wa mpango sheria ambayo kwa Tanzania inakinzana na sheria mbalimbali iliwamo sheria za kimila.

## Wanasayansi chipukizi kuendelea kudhaminiwa

Na Elizabeth Zaya

KAMPUNI ya Shell Tanzania imesema itaendelea kudhamini kazi inayofanywa na Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi (YST), katika kuibua wanasayansi na wabunifu kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya nchi.

Mshauri wa Uhusiano wa kampuni hiyo, Msomisi Mbena, alisema tangu kuanza kwa maonyesho ya kuibua wanafunzi wanasayansi kuanzia mwaka 2011 kutoka katika shule za sekondari mbalimbali Tanzania, kumeongeza ushawishi kwa wanafunzi kupenda masomo ya sayansi tofauti na ilivyo kuwa miaka ya nyuma.

"Tangu YST imeanzisha programu hii, tumeona mafanikio makubwa, kila mwaka idadi ya wanafunzi wanaobuni miradi mbalimbali ya kutatua changamoto ndani ya jamii inaongezeka, hili ni jambo zuri sana na linapaswa kuungwa mkono na kila mtu kwa sababu linasaidia kuleta ushawishi kwa idadi kubwa ya wanafunzi kupenda masomo ya sayansi na tumelishuhudia hilo,"alisema Mbena.

"Na ndio maana tunasema sisi kama Shell Tanzania tutaendelea kusaidia katika hili kwa sababu ni jambo zuri kwa nchi na linapaswa kuungwa mkono na kila mtu au kila taasisi pamoja na serikali."

Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, alisema kupitia programu hiyo, wapo wanafunzi ambao wamekuwa wakipewa tuzo za dhahabu, pesa taslimu pamoja na udhamini wa masomo katika vyuo mbalimbali nchini.

"Tangu programu hii ianze kuendeshwa na YST ni miaka 11 sasa na tumeona mafanikio makubwa, tuna wanafunzi ambao kwa sasa ni madaktari na waliohitimu kwa udhamini kwenye vyuo vikuu mbalimbali kwa udhamini wa mpango huu baada ya kuvumbua miradi iliyowapatia ushindi,"alisema Prof. Mgaya.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchapishaji ya Spreedy, Imran Arab, alisema wao ni miongoni mwa walioona umuhimu wa jambo hilo na kuamua kuunga mkono YST na sasa wanajivunia.

"Wakati tunadhamini jambo hili, hatukujua kama ni msaada kiasi hiki kwa wanafunzi, lakini tumeshuhudia wenyewe na hatujutii kusaidia, tumeona wanafunzi ambao pia ni watoto wetu wamefanya vitu vikubwa ambavyo si tu vitawasaidia wao, lakini vina manufaa kwa nchi, hawa ndio watasaidia katika kutatua matatizo yaliyoko kwenye jamii," alisema Arab.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru (kushoto) na Meneja Mkuu wa Kampuni ya ETC Agro Tractors & Implements Ltd, Praveen Chandra (katikati) wakitia saini mikataba jijini Dar es Salaam jana, yenye lengo la kutekeleza mpango wa kuwakopesha wakulima matrekta na zana mbalimbali za kilimo. Kulia ni Meneja wa masuala ya Utawala wa kampuni hiyo, Mussa Daudi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima kukopeshwa matrekta, zana za kilimo

Na Mwandishi Wetu

SEKTA ya kilimo imepata msukumo baada ya kusainiwa mkataba wa kuwakopesha wakulima matrekta na zana za kilimo.

Mkataba huo ambao lengo lake ni kuiwezesha sekta ya kilimo kupiga hatua, umesainiwa kati ya Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na Kampuni ya usambazaji wa zana za kilimo – ETC Agro Tractors & Implements Ltd.

Akizungumza wakati wa kusaini mkataba huo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, amesema lengo la mkataba ni kuongeza tija kwa wakulima hasa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa.

Alisema NBC kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo katika uchumi wa Tanzania hasa ikizingatiwa inachangia asilimia 30 ya pato la Taifa na kuajiri asilimia 70 ya wafanyakazi wote Tanzania, imeamua kutoa mikopo ya zana hizo kwa wakulima.

"Kwa kutambua hilo tukaona haja kubwa ya kuongeza tija kwa wakulima wetu hawa, kwa hiyo mkataba huu umelenga kuwasaidia wakulima kuongeza matrekta na zana za kilimo ambazo zitaenda kubadilisha kabisa namna wanavyofanya kazi katika kilimo chao," alisema.

Alisema huduma hiyo ya mikopo ya zana za kilimo inatarajiwa kuanza Januari mwaka 2022.

"Matarajio yetu ni kwamba itakuwa ni mkopo ambao una riba nafuu, mkopo ambao una masharti nafuu kwa ujumla.

"Kwa mfano hakutakuwa na dhamana nyingine yoyote. Dhamana pekee itakayotumika ni trekta lenyewe au chombo chenyewe, lakini mkulima atachangia asilimia 25 ya trekta au chombo hicho husika," alisema.

Amesema pia NBC itaangalia mtiririko wa mauzo ya mkulima husika iwapo anaweza kulipa rejesho la mkopo huo au la.

"Kikubwa zaidi marejesho ya mkopo huo yatategemea pia kalenda ya kilimo husika, kwa hiyo kama mtu anafanya kilimo cha mahindi ambalo ni zao la msimu, marejesho yatakuwa wakati wa mavuno.

"Kipindi ambacho mkulima hana mavuno labda anafanya matayarisho ya shamba, mkulima hana haja ya kufanya marejesho, tumefanya hivyo makusudi ili kuwawezesha wakulima kulipa mikopo yao bila kuwa na changamoto yoyote," alisema.

Ameongeza kuwa wakulima wanaweza kwenda kupata mikopo hiyo katika matawi yote ya benki hiyo yaliyopo nchini.

Akizungumzia kwa niaba ya Meneja Mkuu wa ETC Agro Tractors & Implements Ltd, Praveen Chandra, Meneja wa Masuala ya Utawala wa kampuni hiyo, Mussa Daudi, alisema wakulima watakaopata mikopo hiyo ni wale wenye uwezo wa kulima hekari 15 na kuendelea.

Alisema suala la msingi ni kuhakiki na kujiridhisha iwapo mkopaji ni mkulima kweli.

Aidha, amesema, matrekta hayo pamoja na zana nyingine za kilimo zitakopeshwa kwa wakulima kila mkoa kupitia kwa timu ya wataalamu 40 wa kampuni hiyo waliosambaa mikoani. "Mara nyingi tumekuwa tukitoa mafunzo ya awali kabla ya kuwapatia matrekta ambapo huwapatia mafunzo hayo bure kwa siku tatu," alisema.

ama
ALHAMISI DESEMBA 16, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kuibuka kirusi omicron kunavyohimiza ukamilishaji chanjo 'maisha yaendelee'**




Ukurasa 13

**NINI KINAMALIZA MISITU?**

Yalivyo mayowe ya kuangamia tangu Uhuru na ishara ya uokozi



Ukurasa 14

**Uzinduzi Programu Malezi, Makuzi hatua mpya ukombozi afya ya mtoto**

MRADI MIAKA MITANO

# World Vision ilivyoingia ubia na serikali Dodoma, lishe bora, wajawazito, watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MRADI wa 'Mama na Mtoto' unaofadhiliwa na shirika lisilo la kiserikali la World Vision, ukitekelezwa mkoani Dodoma unatajwa kuchangia zaidi katika msukumo wa kinamama vijijini kuhudhuria kliniki na kujali afya ya mtoto.

Inatajwa, kabla ya mradi huo kinamama wengi vijijini walikuwa hawaendi kliniki, hata kuishia kujifungua nyumbani, jambo ambalo ni hatari kwa mama na kiumbe kinachozaliwa.

Baada ya World Vision kuanzisha mradi huo, ikiwamo kutoa vifaa vya msaada hospitalini ili kuwavuta kinamama kuhudhuria kliniki, ni jambo walilofanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na mahudhurio kuwa makubwa.

Hivi sasa imekuwa mithili ya desturi katika vijiji mbalimbali mkoani Dodoma, kuona kinamama wanahudhuria kliniki na watoto wao, wakipima uzito, kupata ushauri nasaha wa lishe bora itakayomsaidia mtoto kukua vizuri kiafya.

Wilaya zinakotekelezwa mradi ni Bahi, Chemba na Kondoa, ambako Nipashe ilizuru kutembelea katika vituo vya wilaya hiyo na kuona kuna mahudhurio mazuri.

### MENEJA MRADI

Daudi Gambo, Meneja wa Mradi wa Afya ya Mama na Watoto wa World Vision, anasema waliamua kuanzisha mradi huo baada ya kubaini watoto wanakabiliwa na utapiamlo kwa sababu wazazi wao hawajui kutengeneza lishe bora, ndio maana wakaona wabuni njia ya kuwasaidia wajawazito na waliokwishajifungua.

Anasema baada ya kufanya hivyo, mwitikio umekuwa mkubwa kwa umma, kwenye maeneo mbalimbali vijijini na anaongeza ndio maana wameamua kujikita katika mradi huo, ili kuwasaidia wajawazito na watoto wanaozaliwa. Anasema lengo walilo nalo ni kuwaona kinamama wote wanahudhuria kliniki na wana uhakika suala litafanikiwa kwa kiasi kikubwa, kutokana na ukweli kwamba kinamama wengi vijijini wanalifurahia mradi huo ambao ni wa miaka mitano.

Meneja anasema, tangu waanze mpaka sasa mwitikio ni mkubwa sana kwa jamii na hasa vijijini, kwa ishara ya wengi wanaohudhuria kliniki katika vituo vya afya kupata huduma za afya zinazotolewa na wahudumu ngazi ya jamii.

### MRATIBU WA MRADI

Joseph Kilimba ni mratibu wa mradi anasema, wakati wanaanza hali haikuwa nzuri kwa sababu kinamama wengi hawakuhudhuria, lakini baada ya mradi huo kusambaa na kueleweka kwa jamii, basi idadi ya watu ilianza kuongezeka katika vituo vya afya, tofauti na mwanzo.

Anasisitiza umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa ajili ya kupata huduma za afya katika ngazi ya jamii, akifafanua kwamba kinachotakiwa kwao ni kuhakikisha wanawaelewesha undani wa mradi, ili kujiweka sawa na familia, kisha kuwasukuma kwenda kliniki kukagua afya zao na watoto.




Ofisa wa taasisi ya lishe na chakula, akieleza jambo mbele ya bango linalohimiza lishe bora kwa watoto na wajawazito, ujumbe unaotekelezwa sasa na mradi wa asasi ya World Vision, mkoani Dodoma. **PICHA: MTANDAO.**

### MJAMZITO AKIRI

Mama Aisha anasema hivi sasa wanahudhuria kliniki kutokana na kwamba wamepata elimu ya kuhudhuria katika vituo vya afya kupima uzito na afya zao kwa ujumla .

Anakiri wengi wao kijijini wanaenda kliniki kufafanua, afya zao pamoja na kupima uzito kwa watoto hao, huku kinamama wajawazito nao wakijitokeza kwenda kupima afya kabla ya kujifungua.

"Tunaishukuru World Vision kwa mradi huu, kwa sababu wametupa elimu ya kutosha kinamama wote wanahudhuria kliniki hivi sasa," anasema Aisha.

Anaipa sifa kwa kauli 'World Vison ndio kila kitu' kwao kutokana na kwamba wamewawezesha wanakijiji kupata elimu ya mama na mtoto, ikiwamo kuhudhuria kliniki.

### JAMII NA LISHE

Kuhusu suala la lishe, World Vision imekuwa ikitoa elimu ya kutengeneza lishe bora kwa watoto, ili kuwasaidia ukuaji na elimu hiyo inawasaidia sana wananchi wa pembezoni, kujua umuhimu wa kutengeneza lishe bora kwa watoto na kinamama.

World Vision imekuwa ikisisitiza kulima mboga za majani pamoja na mimea mingine, ili kusaidia kupata mazao yatayosaidia kutengeneza lishe bora kwa jamii, ndani ya eneo lao.

### OFISA LISHE MKOA

Ofisa Lishe mkoa wa Dodoma, Heriet Carin, anasema wamekuwa wakisisitiza suala la lishe kwa jamii, ili kupunguza utapiamlo kwa watoto wadogo, jambo linalofanyika kila siku kupitia wahudumu wa vituo vya afya.

Anasema, wamekuwa wakishirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha, wanasisitiza suala la lishe bora, ili kutokomeza utapiamlo kwa jamii inayowazunguka.

Heriet anafafanua kuwa lengo lao ni kuona jamii inakuwa vyema hususani kwa watoto wadogo wanaohitaji kukua ndani ya usalama kiafya, ili kufikia ndoto zao, wakitumia zaidi nyenzo ya elimu kwa umma.

AFYA

# Kuibuka kirusi omicron kunavyohimiza ukamilishaji chanjo 'maisha yaendelee'

**Na Michael Eneza**

KUTOJIFUNGIA na kuendeleza shughuli za kiuchumi wakati wa corona, kunaweza kuwa jambo ambalo dunia inaweza kujifunza kutoka Tanzania.

Ni hatua inayoweza kuokoa jahazi, licha ya wasiwasi kuanza kutanda maeneo mengi duniani mwezi uliopita kuhusiana na kusambaa kirusi omicron kilichobadilika kwa kiwango kikubwa.

Hapo kunatajwa, licha ya kusambaa kwake kimataifa kuanzia Botswana hadi Afrika Kusini, bado maisha yanaweza kuendelea bila ya karantini, hata kuokoa jahazi la maisha.

Botswana na majirani Zimbabwe na Eswatini (Swaziland) walifungiwa kusafiri kwenda Ulaya na maeneo mengine, huku taarifa za kuenea kirusi kipya zikisikika karibu kote Ulaya na Asia hadi mwisho wa wiki iliyopita.

Kwanza, kirusi hicho kilileta mshituko mkubwa na kutingisha biashara ya hisa na fedha katika masoko ya fedha Marekani na Ulaya, lakini sasa hali ni shwari.



Wasafiri wakiwa katika uwanja wa ndege nchini Afrika Kusini, wakiwa katika ukaguzi wa maradhi corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**CHANJO YAKE?**

Mambo yamekuwa shwari au kutulia kutokana na maelezo ya awali kuwa, omicron haizuiliwi na chanjo zilizopo hayakuwa sahihi.

Wapo waliodai chanjo inapenya mwilini mwa binadamu na kuleta athari. Kanuni ya msingi inabaki waliopata chanjo wanaambukizwa, ila hawapati maumivu makali na athari nyingi kama wasiochanjwa.

Inaelezwa, baadaye hasa kutoka Israel kuwa waliopata 'chanjo ya pili' au 'ya kuimarisha' (booster), kwa mfano kuongeza chanjo moja kwa waliotumia aina za chanjo ambazo mtu huchanjwa mara mbili, walikuwa salama kwa sehemu kubwa. Ni wasiochanjwa ambao 'omicron' inawaambukiza kwa kasi zaidi.

Ina maana, katika nchi ambazo kampeni ya chanjo zimepiga hatua kubwa, uwapo wa kirusi omicron unaondoa ubishi kuhusu umuhimu wa chanjo imarishi au ya pili, kuwa ni muhimu kwa waliokwishachanjwa.

Sasa mjadala umezuka kuhusu hitaji la aina mpya za chanjo kukabiliana na omicron, kwa madai zilizopo ni kama zinatoa msaada, lakini ni dhaifu kiasi na katika suala hili nako kuna tatizo la kupima chanjo zilizopo zina uwezo gani dhidi ya omicron.

Inavyoelekea ni kwamba, zilizo tayari zilishatajwa kuwa dhaifu na zitakuwa kama kinga za awali tu na si chanjo kamili, kama Sputnik ya Russia na Sinovac ya China. Pia, Saudi Arabia ilikuwa haitambui chanjo hizo kwa wasafiri wa hija waendao Mecca.

> **Rais Cyril Ramaphosa, wiki hii ametangazwa kuwamo katika orodha ya walioambukizwa corona nchini Afrika Kusini.**

Ikiangaliwa hesabu za maambukizi hadi sasa, picha aina tofauti zinajitokeza. Kwanza, ile inayotisha kutoka Wizara ya Afya ya Afrika Kusini kuwa hadi wiki (tatu) zilizopita ilikuwa na wastani wa maambukizi 500 mapya ya corona, lakini omicron ilisababisha kupanda kwa maambukizi hadi 2,800 kufikia mwisho wa mwezi uliopita.

Wizara hiyo ilisema, mwendo huo unaonyesha maambukizi yanaweza kufikia 10,000 ndani ya wiki moja au mbili, ingawa viwango vya ukali wa maambukizi havijaonyesha tofauti kubwa na virusi vya corona.

Kimsingi, kinachoelezwa ni hali tofauti katika protini ya maambukizi (spike protein au ncha ya kirusi) ambayo ni silaha ya kupenya katika chembe za mwili, ili kujijenga na kuumiza.

Ambacho labda kinaleta wasiwasi zaidi kwa wadadisi wa suala hilo barani Afrika na hasa maeneo ya kusini mwa Afrika, ni uwapo wa watu wengi ambao hawajachangamkia chanjo.

Kwa takwimu za maambukizi Afrika Kusini na Ulaya, ni wazi wapo hatarini kuambukizwa haraka zaidi, kuliko ilivyokuwa mwanzoni na yaliyobaki yanakuwa kama mwanzo.

Inatajwa, baadhi ya watu wana kinga zaidi mwilini, wanaugua kidogo na wanapona, lakini wengine hawamudu hasa kama wana mazingira ya kiafya ya kudhoofisha mwili.

Inakuwa mithili ya mtu ana maradhi ya presha (msukumo hasi wa damu), kisukari, udhaifu wa figo au moyo.


Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ametangazwa kuambukizwa maradhi hayo.

Rais Cyril Ramaphosa, wiki hii ametangazwa kuwamo katika orodha ya walioambukizwa corona nchini Afrika Kusini.

Ni jumatatu wiki hii, Rais Ramaphosa, akiwa na mwenyeji wake Rais Macky Sall, jijini Dakar Senegal walieleza kutofurahishwa na namna mataifa kadhaa makubwa kufungia safari za ndege kutoka nchini kwake, kutokana na mlipuko wa virusi omicron.

Rais Ramaphosa, alieleza haja ya mataifa matajiri kushirikiana na mataifa ya chini, katika kusaka suluhisho na si kuziadhibu nchi za chini.

Swali ni kwa kiasi gani kasi ya maambukizi inaweza kupanda tena kwa kiasi cha kutisha? Kimsingi, ilitazamiwa awali Waafrika watakufa sana, lakini haikutokea hivyo. Pia, Afrika Kusini imekuwa na mzigo mkubwa wa corona, kuliko nchi jirani zake.

Kuna wakati Tanzania, kutokana na msimamo wa kisera kutofungia watu ndani, ilianza kuogopwa katika nchi za Afrika Mashariki na Kati, halafu ikathibitika viwango vya corona vilikuwa dhaifu zaidi nchini, kuliko vya nchi hizo.

Hali halisi ni kuwa maambukizi ya corona yalianza kutoweka yenyewe baada ya wimbi kubwa la awali, pasipo kukaa karantini na tangu wakati huo hapajawahi kuwapo wimbi la wazi, ingawa kuna wengi wanatajwa kufariki, kutajwa baadhi ya mikoa kuwapo mlipuko wa juu zaidi.

Kinachogomba ni hatima kama mpangilio wa corona utabaki ulivyo sasa au utabadilishwa na kirusi kipya cha omicron. Ijulikane, majirani wa Tanzania wameendelea kufungiwa ndani, ingawa ni 'lockdown' ya chini isiyofanana na kilichoshuhudiwa Ulaya na Marekani.

Katika mataifa hayo ya Magharibi watu wanalipwa wakiwa nyumbani, wanaletewa bidhaa kutoka sokoni na maeneo yote ya starehe, fukwe zinakuwa nyeupe kukosa wanaojibarizi huko.

Hivyo, hata ndege wasioonekana kwa urahisi wakaanza kujitokeza wakiweka maskani katika majengo marefu ya miji yaliyohamwa na kuanza kuzaliana. Afrika haikuingia katika hali hiyo.

Wataalamu wengine wanadai, kilichotokea hadi sasa kuhusu kirusi omicron, ni kwamba maambukizi ya jumla yanaweza yasiongezeke kwa kiasi cha kushangaza, kwani awali hakikuleta maambukizi kwa kasi ya kutisha iliyotazamiwa na wataalamu Ulaya na Marekani.

Mwaka huu mwanzoni wakati wa wimbi jipya la kirusi cha 'beta, halafu delta' hali hiyo ilijidhihirisha katika maeneo kadhaa.

Ni kwamba mtu anaweza kusema kwa jumla Tanzania imekuwa nchi yenye nafuu katika wimbi la maambukizi ya corona na si kutumia sana barakoa, kuweka umbali, kuacha misongamano inayotajwa kuwezesha nchi kuwa salama.

Tanzania imeshangaza wengine, kuwa watu wake hawachukui tahadhari za wazi, kwa mfano kutojazana uwanjani na ukumbini, wameendelea kusali, wanafunzi kusoma, lakini corona haijawahi kusambaa kwa kina kitaifa.

Wataalamu wa afya nchi za Ulaya, wamejaribu kuelezea hali hiyo kitakwimu na wameshindwa na mara nyingine wamebuni ufafanuzi eti "nchi za Afrika zina uzoefu wa kupambana na magonjwa ya kuambukiza kama ebola, hivyo corona si kitu kigeni kwao."

Ni hoja isiyo na mashiko kitaalamu, kwani usahihi wake walipaswa kusema 'kuna kinga', ingawa bado kunabaki swali ni kinga gani isiyofahamika kwao?

MAZINGIRA

NINI KINAMALIZA MISITU?

# Yalivyo mayowe ya kuangamia tangu Uhuru na ishara ya uokozi

• Kazimzumbwi, hifadhi msitu ulioanzia ukoloni

**Na Dk. Felician Kilahama**

ALHAMISI wiki iliyopita kulikuwapo maadhimisho ya miaka 60 tangu Tanganyika, ilipopata Uhuru.

Pia, Aprili 26 ya mwaka ujao nchi itafikisha miaka 58 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siku ambayo Tanganyika na Zanzibar ziliungana kuunda Tanzania mpya katika ramani ya dunia.

Hicho ni kipindi kirefu kina mengi yaliyotokea, ikiwamo changamoto za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimazingira, ikiwamo ya misitu, moja ya sekta zilizokumbwa na misukosuko mingi tangu kupatikana uhuru wa nchi.

Wakati taifa huru Tanganyika linaundwa, kutoka utawala wa Waingereza walioshika himaya ya nchi tangu kumlizika Vita vya Kwanza vya Dunia, maeneo mengi kitaifa yalikuwa yamefunikwa na misitu na uoto mwingine wa asili, kama mimea na nyasi tofauti.

Nchi ilikuwa kijani na hapakuwapo changamoto ya kupatikana maji, mvua zilinyesha kila wakati na za kutosha, ikilinganishwa na sasa.

Misitu ni sekta iliyogawanyika katika sehemu kuu mbili; miti ya asilia na ya kupandwa.

**UHURU NA MISITU**

Taifa lilipopata uhuru Desemba 9, 1961, hapakuwapo takwimu kamili zilizoonyesha kiasi cha misitu iliyofunika, lakini baadaye jitihada zilifanyika kupima na kutathmini ukubwa wake.

Hapo ndipo kukawepo taarifa za misitu imechukua eneo ukubwa hekta 33.5 milioni, sawa na asilimia 36 ya ardhi yote ya Tanzania Bara.

Wakati wa ukoloni, misitu nchini ilisimamiwa kwa kuzingatia Sera ya Misitu ya Mwaka 1953 na Sheria ya Misitu ya mwaka 1955, pia kanuni zake.

Kwa kutumia vyombo hivyo, wakoloni katika miaka ya 1950, walitangaza na kuanzisha misitu mingi iliyohifadhiwa kisheria (Forest Reserves).

Mathalani ni Misitu ya Hifadhi ya Pugu na Kazimzumbwi iliyoko wilayani Kisarawe mkoani Pwani karibu na Dar-es-Salaam.

Vilevile, wakoloni walishirikiana na utawala wa kijadi, machifu na watemi) na kwa kuwa wataalamu wa misitu walikuwa wachache, hivyo waliwategemea usimamizi wa misitu kufanywa na watawala wa jadi katika maeneo yao na matumizi yake yalidhibitiwa ipasavyo.

Idara ya Misitu hata baada ya uhuru, iiliendelea kusimamiwa na wataalamu wa kikoloni hadi mwaka 1963 serikali iilipomteua raia wa kwanza kuwa Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Misitu.




Mandhari ya Hifadhi ya Msitu Kazimzumbwi, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani. **PICHA: MTANDAO**

> **Kati ya 1961 na 1998, zaidi ya miongo mitatu na nusu tangu Uhuru wa nchi, serikali iliendelea kutumia sera na sheria ilizorithi kutoka mifumo ya kikoloni.**

Baada ya uteuzi huo, juhudi ziliendelezwa kuimarisha usimamizi wa misitu ya asili, mfano hai ni kuimarisha mpaka wa misitu iliyohifadhiwa, pia kuongeza mingine kwa kuitangaza kuhifadhiwa kisheria.

Kati ya 1961 na 1998, zaidi ya miongo mitatu na nusu tangu Uhuru wa nchi, serikali iliendelea kutumia sera na sheria ilizorithi kutoka mifumo ya kikoloni.

Taarifa zinaonyesha wakati uhuru unapatikana, eneo la misitu hekta milioni 16.7 lilikuwa chini ya usimamizi wa kisheria, lakini baadaye ziliongezeka hekta zingine 12,000 ikifanya karibu asilimia nusu ya eneo lote la misitu ikisimamiwa kisheria.

Kadhalika, serikali iliendelea kuisimamia misitu katika maeneo yanayoitwa 'matajiwazi' (Public Land) ikitoa leseni na kukusanya mapato yake.

Baadaye kukawepo kada ya walinzi misitu, hasa katika maeneo yaliyohifadhi kuhakikisha hayaharibiwi, kwa kukata miti au kufyekwa ovyo kwa shughuli za makazi, kilimo na ufugaji.

**UHARIBIFU MISITU**

Pamoja na kuwapo juhudi za kuisimamia misitu, shughuli za binadamu ziliendelea kuongezeka, wakati wa uhuru kulikuwapo Watanzania karibu milioni 10. Kadri miaka ilivyoendelea, idadi ya watu na mifugo iliongezeka, ikiambatana na ongezeko la matumizi ya ardhi na misitu.

**ARDHI KUHARIBIKA**

Ilipofika zama miaka ya 1970, baadhi ya maeneo yalionekana kuathirika kutokana na matumizi yasiyo endelevu. Mfano hai wilayani Kondoa, mkoa wa Dodoma, ambako makorongo kuna makubwa yatokanayo na mmomonyoko mkubwa wa ardhi.

Hapo ndipo kukaanzishwa miradi ya kuhifadhi ardhi katika maeneo hayo na sehemu nyinginezo mkoani Dodoma, ikiitwa Hifadhi Ardhi Dodoma (HADO).

Ilipofika miaka ya 1980 sehemu za Kanda ya Ziwa hususan mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Mara, misitu ilionekana kutoweka kwa kasi kubwa kutokana na kilimo cha pamba, pia makazi.

Vilevile kukashikwa dhana ya kufyeka misitu kwa lengo la kufukuza nzi mbun'go wanaoambukiza malale na kuzuia magonjwa kwa mifugo.

Ni hali iliyoathiri ustawi wa misitu na uoto asili, hata matokeo yake yakawa ni uharibifu mkubwa wa ardhi na hata maeneo ya mkoa wa Shinyanga kugeuka jangwa.

Mwaka 1984 kulifanyika mkutano uliohudhuriwa na viongozi wa kitaifa na Rais Julius Nyerere, akiwa mwenyekiti, mkutano ukaazimia kuanzishwa Mradi wa Hifadhi Ardhi Shinyanga (HASHI), kwa lengo la kuokoa ardhi na kudhibiti matumizi yasiyo endelevu.

Pia katika miaka ya 1970, Idara ya Misitu ilianzisha upandaji miti na kuwaelimisha wanavijiji kupanda miti.

**SERA MPYA**

Mwaka 1998, sera ya misitu ya kikoloni ilibadilishwa, utunzaji misitu na upandaji miti ukapewa msukumo zaidi, hata kuvifanya vijiji viwe vitovu vya hifadhi ya misitu ya asili kupitia mkakati wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.

Hata hivyo, ongezeko la watu na kufutwa kada ya walinzi misitu kulisababisha usimamizi misitu kudorora. Vilevile, serikali ilifuta utawala wa kijadi ambao kwa kiasi ulilinda misitu isiharibiwe ovyo.

Ni mazingira yaliyoendana na kuibuka tabia misitu ionekane rasilimali isiyokuwa na mwenyewe kutokana na usimamizi duni, pia matumizi ya bidhaa za misitu.

Ushuhuda wake unapatikana kwenye kuni na mkaa zikawa zaidi ya asilimia 90 ya nishati itumikayo nchini, kadhalika kasi ya uvunaji miti ikawa kubwa na kusababisha misitu ya asili kutoweka kwa kasi kubwa kila mwaka.

Vivyo hivyo, kukawapo makazi na kilimo cha kuhamahama katika himaya ya hifadhi ya misitu.

**KUTOWEKA MISITU ASILIA**

Katika misitu asili hata baada ya kuanzisha Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) mwaka 2010, kasi ya kupoteza misitu ya asili imeendelea kuwa kubwa, ikitokana na ukweli kwamba Idara ya Misitu, pamoja na wakala huo haina uwezo wa kudhibiti uharibifu.

Ni zama misitu ya asili ikageuka 'shamba la bibi' kwa kukosa ulinzi, watu wakafanya wanavyotaka, hata takwimu zinaonyesha kutosimamiwa vyema misitu ya asili, iliofanya hata kufika mwaka 2015, hekta 372,000 zilikuwa zinatoweka kila mwaka.

Vilevile, Kituo cha Kufuatilia Masuala ya Hewa Ukaa (carbondioxide) kilichoko katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) mwaka 2017 kilionyesha kasi ya kutoweka misitu ni kubwa wastani hekta 469,420 kwa mwaka, huku inayoharibika ikiongezeka katika mikoa ya Magharibi.

Ikiunganishwa na ukataji miti kiholela kwa ajili ya kilimo cha kuhama, kuchoma mkaa, mifugo, kupata kuni, mbao na kujenga makazi na vitega uchumi, athari zake kimazingira ni kusababisha hali ya maisha magumu kwa kukosekana mvua, ukame, mmomonyoko wa udongo, kukosa nishati, mafuriko na kukosekana mapato ya serikali kuu, pia vijiji.

**• Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki Mstaafu.**

AFYA

# Uzinduzi Programu Malezi, Makuzi hatua mpya ukombozi afya ya mtoto

**Na Maulid Mmbaga**

- Inabeba jukumu lenye ajenda afya kitaifa
- Rais, Waziri Mkuu na Waziri Afya wanena



Chakula chenye lishe bora. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

SUALA la lishe bora kwa Watanzania hususani mjamzito na mtoto, linatajwa bado ni kubwa hata kuchangia udumavu wa akili na kimwili, ikirudisha nyuma maendeleo ya watoto nchini.

Kutokana na hilo, serikali imeendelea kusisitiza mamlaka husika na wadau mbalimbali wa afya na lishe kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuijengea uelewa wa umuhimu huo wa lishe sahihi, ili kuwa na taifa lenye nguvukazi imara.

Ni umuhimu ambao kisera unachangia maendeleo ya uchumi nchini na imepewa kipaumbele, pia kuwekewa mikakati ya utekelezaji katika malengo, mipango na maandiko ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Hapo inajumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030; Malengo ya Baraza la Afya Duniani ya Mwaka 2025; na Ajenda ya Afya ya Mwaka 2063.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya mtoto, Desemba 13 mwaka huu imezindua Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

Ni programu inayotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ikiwa na dhumuni la kuhakikisha kunakuwapo elimu lishe bora na makuzi ya mtoto inatolewa kwa jamii yote nchini.

### HATUA ZAKE

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Mkuu wa Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Mwajuma Magwiza, anasema ukosefu wa lishe bora unaangukia ukatili wa watoto, kwani unawasababishia udumavu wa akili na mwili, anasema jambo ambalo si salama kwao.

Mwajuma anasema, siku chache zilizopita jijini Dodoma amefungua mafunzo kuhusu Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, kwa wataalamu wa sekretarieti za mikoa nchini.

Anasisitiza jamii inapaswa kufahamishwa namna bora ya malezi kwa watoto wao, katika kila hatua kitaalamu, ili kuwajengea watoto misingi imara ya ukuaji na kujifunza.

“Kuna hatua za malezi za kitaalamu ambazo jamii zinapaswa kujengewa na washiriki wote, kutokana na utaalamu wenu. Huduma za malezi zinatakiwa zimjengee mtoto afya, lishe, kujifunza na mwitikio.

> **“Kuna hatua za malezi za kitaalamu ambazo jamii zinapaswa kujengewa na washiriki wote, kutokana na utaalamu wenu. Huduma za malezi zinatakiwa zimjengee mtoto afya, lishe, kujifunza na mwitikio.**



Mtoto mwenye lishe duni.

“Hivyo, kuanzishwa programu hii kutasaidia, kwani kunawajumuisha wataalamu wakiwamo madaktari ambao wana sayansi ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. Hivyo watatusaidia katika kuelimisha jamii,” anabainisha Magwiza.

### DIRA YA VIONGOZI

Rais Samia Suluhu Hassan, alipowahutubia wananchi jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru, anataja lishe ina nafasi kubwa katika kujenga watoto wenye afya bora, akisisitiza haja ya kuwapo uboreshaji afya za watoto.

“Bado kazi ya kuhakikisha Taasisi ya Chakula na Lishe inatoa elimu bora ya lishe kwa watoto, kwa kipindi chote cha ujauzito hadi miaka mitano. Ina umuhimu kuendelea kutolewa, ili kuhakikisha kiwango cha udumavu kwa watoto kinashuka,” anasisitiza Rais Samia.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mtoto, Sebastian Kitiku, anawataja wadau wanaoshirikiana nao kutekeleza ajenda hiyo wanajumuisha maofisa lishe, elimu, maendeleo na ustawi wa jamii na waganga wakuu wa mikoa.

Anasema, programu hiyo inategemea ushiriki wa serikali kutekeleza mipango yake na kushirikiana na wadau mbalimbali.

Programu ilizinduliwa tarehe 13, mwezi huu na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, akiipongeza Taasisi ya Karibu Tanzania Organization (KTO) kwa kutoa wataalamu watakaosaidia kufanikisha suala hilo.

Anasema utoaji huduma inapaswa kuendana na malengo ya baadaye, pia kuzalisha wataalamu watakaosaidia. Waziri Gwajima anafafanua: “Naamini kuwa wanaofundishwa, watakuwa chachu ya kuzalisha watu wenye uelewa na faida kwa nchi.”

### MALENGO SERIKALINI

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati anahutubia Mkutano wa Saba wa Wadau wa Lishe uliofanyika tarehe 18 mwezi uliopita jijini Tanga, anasisitiza serikali imedhamiria kuendelea kuipa umuhimu zaidi wa suala la lishe nchini, ili kuhakikisha kunakuwapo uchumi imara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Dk. Germana Leyna, anasema kiwango cha udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano kimepungua kutoka asilimia 34.7 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018.

Dk. Leyna anasema Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 1995, iliainisha kiwango bado kinaashiria hali mbaya ya lishe nchini na inakadiriwa kuwa kuna kiwango cha watoto zaidi ya milioni tatu waliodumaa.

“Idadi kubwa ya watoto iko mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Kigoma, Tanga, Ruvuma, Geita, Kagera, Morogoro, Tabora na Mara. Kiwango cha ‘ukondefu’ kimepungua kutoka asilimia 3.8 mwaka 2014 hadi asilimia 3.5 mwaka 2018.

Anafafanua kwamba, uzito uliokithiri kwa wanawake walio na umri wa uzazi limeongezeka kutoka asilimia 29.7 mwaka 2014 hadi asilimia 31.7 mwaka 2018; na mikoa inayoongoza ni Mbeya, Arusha na Kilimanjaro.

Mtaalamu huyo anafafanua uzito uliokithiri unachangia magonjwa sugu yasiyoambukiza yanayosababishwa na lishe isiyo sahihi na mtindo mbaya wa maisha, ingawaje anawatetea wanajitahidi kudhibiti tatizo la udumavu na utapiamlo.

### KUTOKA UNICEF

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), linasema lishe bora na huduma za msingi kama elimu na afya ni haki ya kila mtoto.

Taarifa yake inasema kutokana na hilo, inaendelea kushauri na kusisitiza wazazi na walezi kuhakikisha wanazingatia malezi na lishe bora, kwa watoto wao ili kuwasaidia kuwa na mlolongo mzuri katika hatua za makuzi.

### WANENAYO WANANCHI

Hidaya Shabani, mama wa watoto wawili na mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, anaeleza kuridhishwa na kuanzishwa programu hiyo akiwa na ufafanuzi itasaidia kuielimisha jamii na utekelezaji sahihi wa jukumu la malezi bora kwa watoto.

“Mafunzo hayo yatawajenga na kuwakumbusha umuhimu wa malezi sahihi kwa watoto, kwani ni muda mrefu watu wamekuwa kama wamejisahau.

“Pia, nitoe wito kwa walezi na wazazi wenzangu elimu hiyo itakapowafikia waweze kuizingatia kwa faida ya kizazi kilichoko na kijacho,” anashauri Hidaya.

# Rasimu ya viwango vya mbegu sasa yaandaliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Uthibitisho Rasmi wa Mbegu Tanzania (TOSCI) imeandaa rasimu ya viwango vya uidhinishaji wa mbegu za mazao mbalimbali ya miti katika hatua inayolenga kuboresha sekta ya kilimo.

Mazao ya miti husika ni parachichi, kahawa, chai, korosho, mawese, zabibu, machungwa, maembe pamoja na mapapai.

Akizungumza wakati wa mahojiano maalumu na gazeti hili jijini Dodoma, Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema rasimu hiyo iliyoandaliwa itajadiliwa kwanza na wadau wa mbegu hapa nchini.

"Katikati ya mwezi huu, wadau muhimu katika sekta ya mbegu wanatarajia kukutana katika mkutano wa kitaalamu ambao miongoni mwa mengine, utajadili rasimu ya viwango vya uidhinishaji vya mbegu/miche iliyoendelezwa," alisema.

Aliongeza kuwa, baada ya kuthibitishwa na wadau na wataalamu wa kilimo, viwango hivyo vitawasilishwa Wizara ya Kilimo ili kupata baraka na idhini ya mwisho.

"Hii itahakikisha wakulima wanaojihusisha na kilimo cha mazao hayo ya miti ya kiuchumi katika mikoa mbalimbali wanapatiwa mbegu/miche iliyoboreshwa ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi," alisema Ngwediagi.

Aidha, alisema chombo hicho cha udhibiti wa mbegu kitashirikiana kwa karibu na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ili kuhakikisha wakulima wa ndani wanapata aina ya mimea ya kutosha na iliyoboreshwa kwa mazao yote muhimu ya chakula na kiuchumi yanayolimwa nchini.

Ikiwa na makao yake makuu mjini Morogoro, TOSCI sasa inatambulika kimataifa baada ya kuthibitishwa na Shirika la Kimataifa la Kupima Mbegu (ISTA), pamoja na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) kwa ajili ya uhakiki wa vyeti vya aina mbalimbali za mbegu nchini.

Kwa sasa, mbegu zinazokaguliwa na kuthibitishwa na TOSCI zinaweza kuuzwa nchini na ziada kusafirishwa kwenda nchi nyingine.

TOSCI ina jukumu la ukaguzi wa mashamba ya mbegu, uchukuaji sampuli za mbegu, upimaji wa mbegu, tathmini ya aina na uhakiki kupitia majaribio ya kitaifa ya utendaji (NPT), majaribio ya utofauti wa mbegu, usawa na uthabiti (DUS) na majaribio ya viwanja vya udhibiti.

Tanzania pia ni mwanachama wa Umoja wa Kimataifa wa ulinzi wa aina mpya za mimea (UPOV), tangu mwaka 2015.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akiongoza kikao cha wataalamu kutoka wizara hiyo na wawekezaji wa Kampuni ya Tree Global, jijini Dodoma jana, chenye lengo la kuingia makubaliano kati ya serikali na kampuni hiyo katika upandaji wa miti ya korosho na cocoa kwa ajili ya kutunza mazingira na kupunguza umaskini. Wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Gregory Hess. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## UMATI yafichua kiini watoto wenye ulemavu kukosa haki

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

CHAMA cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI) kimesema uelewa mdogo kwa wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu umewasababishia wengi kukosa haki zao za msingi.

Aidha, tabia ya wazazi na walezi kuwaficha watu wenye ulemavu majumbani imechangia kwa kiasi kikubwa kuwa maskini na kushindwa kujiamini kama watu wengine wasiokuwa na ulemavu.

Ofisa Mradi wa UMATI Mkoa wa Dodoma, Joyce Deemay, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema uelewa mdogo walionao wazazi na walezi wenye familia hizo zenye watu wenye ulemavu, umechangia kwa kiasi kikubwa kuwa na umaskini uliokithiri.

Aliwataka watu wanaoishi na wenye ulemavu hao kuachana na tabia hiyo kwa kuwa ni ukatili na unyanyapaa, unaowakosesha kupata haki zao za msingi kama ilivyo kwa wengine wasiokuwa na ulemavu.

"UMATI inawaomba wazazi na walezi kutowafanyia ukatili wa kutowapatia huduma mbalimbali wanazostahili kupata zikiwamo za kiafya na elimu kwa wenye ulemavu hao, ambao wanaishi nao kwenye familia zao," alisema.

Alisema, chama hicho kimekuwa kikihakikisha kinatoa huduma za kiafya kwa kuwafikishia kwenye maeneo yao wanayoishi.

Alisema tatizo lililoko ni baadhi ya wazazi na walezi hawatoi ushirikiano wa karibu suala ambalo limesababisha walio wengi kujikuta wakikosa matibabu.

# Redio za kijamii zashauriwa maudhui ya maadili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

REDIO za kijamii zimetakiwa kuendelea kuandaa maudhui yanayozingatia maadili na miiko ya Kitanzania.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Magharibi, Emmanuel Buhohela, alipokuwa kifungua kongamano la redio za kijamii jijini Dodoma juzi.

Kongamano hilo lililoandaliwa na Mtandao wa Redio za Kijamii Tanzania (TADIO), Mtandao wa Kutoa Huduma za Redio Afrika Mashariki (EARS) na Shirika la Habari la Kuchochea Mabadiliko la Ujerumani.

Alisema serikali inathamini sana umuhimu wa vyombo vya habari hasa redio za kijamii ambazo zinawafikia watu wengi hasa sehemu za vijijini.

Alizitaka redio za kijamii kuendelea kuandaa maudhui yanayozingatia maadili na miiko ya kitanzania.

Alisema mchango wa redio za kijamii ni mkubwa kwani wananchi wengi wanafikiwa na redio hizo zimekuwa ni sehemu muhimu sana za kusambaza taarifa na ni ukweli ulio wazi kwamba uandishi wa habari zinazojali maisha na kero za watu huchangia kwa kiasi kikubwa kujenga uwelewa na kupunguza umaskini.

"TADIO mnafanya kazi kubwa sana, nimeambiwa mtandao wenu unawafikia asilimia 70 ya Watanzania hasa waliopo vijijini, haya ni mawanda makubwa sana ya kuifikia jamii kimawasiliano," alisema.

Alisema kuna changamoto nyingi zinazozikabili redio za kijamii zikiwamo uwezo mdogo wa kifedha, uwezo wa kitaaluma miongoni mwa watendaji. changamoto ya tozo na kodi mbalimbali.

"Niwahakikishie kwamba serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba tasnia ya habari inakua hasa maendeleo endelevu ya redio za kijamii ... kwa hili naomba tukae pamoja, tutafakari na tupange mipango ya pamoja ya kuwa na mipango endelevu ya kuziimarisha redio zetu na kuondoa vikwazo," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa TADIO, Baptist John, alisema uanzishwaji wa redio jamii sio rahisi na changamoto iliyopo ni uendeshaji na kuwezesha waandishi kuwa na mapato yanayojitosheleza ili kuwasaidia wasiwe wanapotosha taarifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la habari la M'CT la nchini Ujerumani, Klaas Grinwinkel, alisema redio za kijamii zikipewa ushirikiano na kuwezeshwa zina mchango mkubwa sana katika kuhabarisha jamii.





# Mradi wa bil. 200/- kuleta fursa ya maji jijini Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imetenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji, ambao chanzo chake ni kutoka Mto Kiwira wilayani Rungwe.

Utekelezaji wa mradi huo utawezesha utoaji huduma ya maji kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na maeneo mengine.

Usanifu wa mradi umeanza na kwamba hadi kukamilika kwake, utachukua miaka miwili ili wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuondokana kabisa na adha ya kukosa majisafi na salama.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (UWWAS), Gilbert Kayange, alisema ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza Machi 2022.

Kayange alisema mradi huo ukikamilika utazalisha maji lita milioni 125 kwa siku na huduma hiyo kuwafikia watu 850,000 kila siku.

"Uwapo wa mradi huo itakuwa mwarobaini kwa wananchi kuondokana na tatizo la ukosefu wa maji jambo ambalo litasaidia kupata majisafi na salama kwa wakati, tunaendelea kutekeleza miradi mingine katika wilaya za Chunya, Mbarali, pamoja na Mlowo mkoani Songwe ili kuwasaidia wananchi kupata huduma za maji na kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali," alisema Kayange.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edna Mwaigomole, aliwahakikishia wananchi mkoani Mbeya kupata huduma ya majisafi na salama kutoka katika vyanzo mbalimbali ukiwamo Mto Kiwira, ambacho kitamaliza tatizo la rasilimali hiyo kutokana na ukubwa wa mradi.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, akizungumza na wakazi wa Kitongoji cha Mpenjele, baada ya kukagua ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa vinavyojengwa katika Shule Shikizi ya Igala, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbadala masomo wakati wa likizo wapatikana

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SIKU chache baada ya serikali kupiga marufuku masomo ya ziada kwa wanafunzi wanapokuwa likizo, uongozi wa Shule ya Wasichana ya bweni ya Joyce iliyopo kijiji cha Ntokele wilayani Rungwe, umeandaa programu maalum ya ufundishaji kwa kutumia mitandao ya kijamii wa Whatsapp kupitia simu za wazazi au walezi wao.

Meneja wa Shule hiyo, Augustino Tweve, alisema jana kuwa wameona ni vyema kufanya hivyo ili kuwaweka wazazi kuwa jirani na wanafunzi na kufuatilia mienendo yao na kufahamu uelewa katika masomo kwa kiasi gani.

"Baada ya serikali kutangaza kusitisha masomo ya ziada kama uongozi wa shule, tukaona licha ya kuwapatia mitaala ya kujisomea nyumbani pia ni vyema wazazi wawajibike kwa namna moja ama nyingine kwa watoto wanapokuwa likizo kwa kuwatumia maswali na kuyafanya na kuyarejesha kwa walimu kwa ajili ya kusahihisha na kurejeshwa majibu," alisema Tweve.

Alisema kutokana na mitaala ya elimu kutofautiana kati ya shule binafsi na serikali, alishauri shule za serikali kuangalia namna ya kuandaa vipindi wakati huu wa likizo ili kutengeneza mazingira ya kuwandaa wanafunzi inapofika Januari waweze kufanya vizuri zaidi katika masomo.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Award Mpandilah, alisema wamelazimika kuwa na mfumo huo kwa kutambua kuwa kwa sasa sekta ya elimu ina ushindani mkubwa hususani kwa shule binafsi.

Mmoja wa wanafunzi, Clara Mgimba, alisema kipindi hiki cha likizo watajikita zaidi kujisomea na kuepukana na makundi ili kutimiza ndoto zao na kutangaza elimu ya mtoto wa kike na manufaa yake.

Alisema licha ya kupewa elimu ya darasani, pia wamekuwa wakifundishwa elimu ya kujitambua na namna bora ya kuepukana na vikwazo ili kuwasaidia watoto wa kike kusoma kwa bidii na kufikia malengo waliyoyakusudia.

# Vyombo vya kisheria vyaombwa kudhibiti ukatili wa kujinsia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani Mbeya vyombo vya kisheria vinavyotoa maamuzi vimetakiwa kutenda haki ikiwamo kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaohusika.

Baadhi ya madiwani mkoani Mbeya kwa nyakati tofauti walisema moja ya majukumu yao ni kuhakikisha vitendo vya ukatili wa kijinsia vinakomeshwa kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu pale inapothibitika na mamlaka za kisheria.

Akizungumza juzi wakati wa kikao cha kujadili kwa namna gani viongozi wa kisiasa wanashiriki kutokomeza vitendo hivyo wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Diwani wa Igurusi, Hawa Kihwele alisema mbali na kutoa elimu, lakini baadhi ya sheria zinapaswa kurobeshwa.

Alitaja sheria hizo kama vile ya mtoto ambayo bado haijabainisha mtoto mwisho miaka mingapi hali inayochangia kundi hilo kujiingiza kwenye ndoa za utotoni au ajira katika maeneo mbalimbali.

"Vitendo vya watoto kubakwa vimeshamiri katika jamii zetu na unakuta vithibitisho vyote vipo lakini baadaye unakuta mtuhumiwa achukuliwi hatua zozote za kisheria ujamaa na undugu unaingia hapo," alisema Kihwele.

Aidha, alizungumzia wanawake wanaonyanyaswa kwenye ndoa, vipigo na ukatili wa kiuchumi aliwahamasisha kwenye vyombo vya sheria kudai haki zao huku akiwaomba waandishi wa habari kuendelea kuandika na kuibua vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii ili vikomeshwe.

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Elimisha, Festo Sikaganamo, alisema kumekuwa na idadi kuwa ya wanawake kufanyiwa vitendo vya ukatili na kwamba moja ya sababu ni wenzi wao ambao ni wanaume kunywa pombe kupitiliza na kusababisha vipigo kwa wake zao na wakati mwingine kutelekeza familia zao.

Alisema katika kukabiliana na vitendo hivyo, Shirika la Elimisha linaendelea kutoa elimu ya athari za ukatili wa kijinsia sambamba na kuwafundisha masuala ya ujasiriamali ili kila mmoja afanye shughuli itakayomwingizia kipato.





# SMZ kuboresha makazi matabibu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imesema katika mwaka 2021/22 imejipanga kuboresha makazi bora ya madaktari wakiwamo wanaofanya kazi katika hospitali za vijijini.

Imesema mpango huo unakwenda sambamba na ujenzi wa hospitali za mikoa na wilaya.

Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mwakilishi huyo alitaka aliyetaka kujua mikakati ya ujenzi wa nyumba ya daktari katika kisiwa kidogo cha Kojani kwa kuwa iliyopo sasa si rafiki kwa makazi ya daktari.

Mazrui alisema mikakati ya wizara ni kuhakikisha wafanyakazi wake, wakiwamo madaktari, wanafanya kazi katika maeneo rafiki pamoja kuwa na makazi yenye heshima ambayo yatawaweka katika utulivu wa hali ya juu.

Alikiri nyumba ya daktari katika kisiwa hicho ni mbaya na kwamba juhudi za makusudi zinahitajika kuchukuliwa ili kuwafanya madaktari kutoa huduma zao katika visiwa vidogo vidogo vilivyoko Pemba.

Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, wizara imejipanga kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa vituo vya afya vijijini pamoja na hospitali katika wilaya za Unguja na Pemba huku nyumba za madaktari zikijumuishwa.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu kuhakikisha tunajenga hospitali katika kila wilaya katika mwaka wa fedha 2021/22 na kujenga nyumba za madaktari ambazo zitawawezesha kutekeleza majukumu yao katika mazingira mazuri," alisema Mazrui.

# Zanzibar, Uingereza zaungana mapambano ya dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR na Uingereza zimetiliana saini hati ya makubaliano na ushirikiano katika kupambana na dawa za kulevya.

Hati hiyo imetiwa saini na Mwakilishi kutoka Uingereza Simon Charters na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, Kanali Burhan Zubeir Nassor.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana Ikulu mjini Zanzibar na kushuhudiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kanali Nassor, alisema makubaliano hayo yatajengea uwezo Zanzibar kupambana na dawa za kulevya.

Mkurugenzi huyo alitoa onyo kwa wanaojihusisha na dawa za kulevya sasa kuwa watakamatwa kwa kutumia teknolojia za kisasa na serikali imejipanga kutokomeza biashara hiyo.

Alisema wamekuwa na washirika wengi katika kupambana na dawa za kulevya na wanatarajia kupokea vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuimarisha mapambano hayo na vitafungwa katika bandari zote.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, pia wafanyakazi wa tume hiyo watajengewa uwezo wa kupeleleza na kujua wanaojihusisha na dawa za kulevya walikojificha, hivyo kuwafichua.

"Nichukue fursa hii kuwaambia wote wanaojishughulisha na biashara haramu ya dawa za kulevya waachane nayo kwa sababu tumejipanga vizuri kuhakikisha Zanzibar bila dawa za kulevya inawezekana," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kuwa na ushirikiano na tume hiyo katika kutoa taarifa na mtoa taarifa atalindwa na taarifa zake zitakuwa siri ili kuokoa jamii ya kizanzibari.

Naye Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, alisema nchi yake ina ushirikiano mkubwa na Zanzibar katika nyanja mbalimbali zikiwamo biashara na elimu kwa kutoa nafasi za masomo.

Alisema mkataba waliotia saini ni kwa ajili ya kupambana na uhalifu wa kimataifa kuhusu dawa za kulevya ambao umekuwa ukiongezeka.

"Njia pekee ya kubambana na uhalifu huo ni kuunganisha nguvu za pamoja katika suala hili ili kutokomeza vitendo vya uhalifu. Hakuna nchi inayopambana na uhalifu huo bila kuunganisha nguvu za pamoja ndiyo maana nchi yangu imetiliana saini makubaliano na Zanzibar," alisema Balozi Concar.

Alisema wataalamu kutoka Uingereza watakuja Zanzibar kwa ajili ya kusaidiana mbinu za kupambana na uhalifu ili kuifanya Zanzibar kuwa salama na kuwavutia wawekezaji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Salum Mkuya, alisema wiki ijayo wanatarajia kubadilisha sheria ya dawa za kulevya kutoka tume na kwenda katika mamlaka ambayo itakuwa na nguvu kisheria kupambana na biashara hiyo.



Msongamano wa abiria ndani ya meli ya Ikram, ikiwa safarini kuelekea kisiwani Pemba jana, ambapo usafiri huo umekuwa wa shida kutokana na idadi ya wananchi wengi wanaosafiri hasa kipindi hiki cha Desemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Hemed Suleiman ahimiza viongozi kuheshimu sheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa sekta mbalimbali wametakiwa kuheshimu sheria za utumishi wa umma katika majukumu yao ili kusimamia misingi ya utawala bora.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo jana wakati akifungua kongamano la nne la kitaifa la utawala bora lililofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdulwakil, Kikwajuni mjini hapa.

Alisema ni vyema watendaji wakaachana na vitendo vyenye uvunjifu wa misingi ya utawala bora vikiwamo rushwa, kutokuwa na mwenendo mzuri wa kimaadili, na kuwataka kufuata sheria za utumishi wa umma na sheria zote zilizowekwa na serikali kupitia katiba.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi kukiuka sheria na taratibu za kiutumishi ikiwamo kuchelewa kuingia kazini, kuondoka kabla ya muda na udanganyifu jambo ambalo linazorotesha utendaji wa kazi katika ofisi za umma.

Hemed alisema utawala bora ni suala linalozingatia misingi ya ufanisi wenye tija na kwamba ni matarajio kongamano hilo litaamsha ari na hamasa ya kuimarisha utawala bora ndani ya Zanzibar.

"Napenda nikukumbushe kuhusu suala la utawala bora kwamba ni suala linalozingatia misingi ya ufanisi na tija, utawala wa sheria na haki za binadamu, ushirikishwaji, kuzuia rushwa, kuzingatia maadili na uadilifu, uwajibikaji na uwazi na kuzingatia matakwa ya wananchi," alisema Hemed.

Alisema serikali imeanzisha taasisi mbalimbali kama Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa ajili ya kuimarisha na kusimamia maadili ya viongozi na wa utumishi wa umma lengo likiwa ni kuimarisha utawala bora.

Hemed alisema taasisi na makundi mbalimbali yana wajibu katika kuheshimu na kuimarisha maadili, haki za binadamu, uwajibikaji na kupiga vita rushwa ili kusimamia haki na wajibu kwa wananchi wanaotaka huduma.

Alisema katika kupunguza vitendo vya rushwa, serikali imeweka mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki kwa taasisi za serikali ili kuimarisha uwajibikaji na kuzuia vitendo vya rushwa katika taasisi za umma.

Hemed aliwataka viongozi waliopewa dhamana kujitahidi kuwa wabunifu katika kupanga na kutekeleza mipango iliyopo ili kuendeleza jitihada zinazochukuliwa na serikali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, aliwakumbusha viongozi kusimamia haki za wafanyakazi na kuhakikisha wananchi hawadhulumiwi katika maeneo yao ya kazi.

Haroun alisema Taasisi ya Huduma za Sheria (LSF) imekuwa kichocheo cha utawala bora katika utendaji na usimamizi wa masuala ya sheria. Alitumia fursa hiyo kuiomba Taasisi ya LSF kuisaidia mahakama ili kesi ziweze kuhukumiwa haraka na kuondokana na mrundikano wa kesi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA.

NYUMBA YA GOROFA INAUZWA IPO UKONGA,INAFREM NANE ZOTE ZINA WAPANGAJI,INAFAA KWA MAKAZI AU BIASHARA,BEI MAELEWANO(WAWEZA LIPA KWA **AWAMU) SIMU.0715 244754**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA



**FABRICE OSCAR CYUBAHIRO**

RAIA WA RWANDA AMBAYE PICHA YAKE IMEONESHWA HAPO JUU, MWENYE PASPORT NAMBA RWA. PC 504353
ANAOMBA URAIA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, AMEISHI NCHINI TANGU MWAKA 1987 KATIKA MIKOA YA KAGERA NA SHINYANGA AKIJISHUGHULISHA NA BIASHARA.
MTU YEYOTE MWENYE SABABU YA KUPINGA MWAOMBAJI ASIPEWE URAIA, ATUME TAARIFA YAKE KWA MAANDISHI ILIYOSAINIWA KWA KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI S.L.P. 512 DAR ES SALAAM.

..........................................
**K.n.y. KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI**

## KUPOTEA KWA CHETI



MONICA EMMANUEL MUNISHI anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1943-0044 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MAGOZA mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DAR/STA/RB/806499/2020

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VALENTINE LEOPOLD NDANU**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T125BEL** Chassis namba **01250318** Engine namba **5759970** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu Taarifa ya Polisi – **ARU/ARU/RB/588886/2021**

……………………………
**ON BEHALF OF COMMISIONER GENERAL OF IMMIGRATION**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Mahakama ya mwanzo………….MKUMBURU**
**wilaya ya HANDENI**
**MADAI NAMBARI 40 YA 2021**
**Mdai ASIFIWE WILLIM WA MAZAGARA**
**Mdaiwa RAJABU HAMISI WA SEGERA**
**Kwakuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake kwamba UNADAIWA TSH 430,000/= LAKI NNE NA ELFU THELATHINI ZA BIDHAA DUKANI**

Kwahiyounahitajiwa kuhudhuria bbinafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 30 mwezi desemba/2021 saa 8;30 asubuhi kwakujibu madai hayo,na kwakuwa sikun hiyo ni siku ya kukata shauri ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itathibitika kama umepokea kuitwa shauri hili ,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa .
Hati hii imetolewa kwa amri ya mahakama hii leo tarehe 8 desemba/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndugu SALEHE ALLY HEMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISHI ROSA yenye namba za usajili T.510 BYT. Chassis namba BE63EG101308. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **KOR/RB/572/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndugu SALEHE ALLY HEMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISHI CANTER yenye namba za usajili T.884 DEL. Chassis namba FE648E520376. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **KOR/RB/572/2021.**

**ABA-JAJA COMPANY LIMITED**

**TAARIFA/NOTISI**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA KAHAMA**
**ILIYOPO KAHAMA**

**SHAURI LA JINAI NAMBA 193/2020**
**JAMHURI…………MLALAMIKAJI (M/S BHUMI RESOURCES TANZANIA LIMITED)**

**V/S. MSHITAKIWA…………….THOMAS JUMA BRASHI**

**Kwa: THOMAS JUMA BRASHI,**
Unaarifiwa kuwa nimepata hati ya kukamata mali dhidi yako katika shauri la jinai namba 193 ya 2020 ya Mahakama ya Wilaya Kahama iliyopo Kahama, unaarifiwa kuwa ulipe Sh. 35,000,000/= kwa ajili ya mlalamikaji – M/S Bhumi Resources Tanzania Limited ndani ya siku kumi na nne (14) tangia siku ya kutolewa kwa taarifa (Tangazo) hii pamoja na gharama za ukazaji hukumu. Usipotekeleza hatua nyingine za ukazaji hukumu zitaendelea dhidi yako bila taarifa/notisi nyingine kutolewa kwako.

C. R. Kabenga
Dalali wa Mahakama
SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RUFINA ISACK MWACHA**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T480 CZV, Engine No.1AZ-FSE Chassis No. AZR65-0124967 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/477034/2021. Imeripotiwa na .GIDEON ELPHAS MATHAYO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA

## MIAKA 60 YA UHURU

# Uhaba wa wataalamu wa ardhi ulivyoundiwa mkakati kuutatua

**Na Mwandishi Wetu**



Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro, Haruna Lugalla, akitoa ufafanuzi namna vifaa vya kisasa vya upimaji vinavyotumika wakati wa mahafali ya 40 ya chuo hicho yaliyofanyika Novemba 26, mwaka huu. Kushoto ni Mary Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MWANZONI mwa miaka 1970, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alianzisha Operesheni Vijiji iliyolenga kuwapanga wananchi kukaa kwenye vijiji ili kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii.

Hadi leo ukipita kwenye vijiji vilivyoanzishwa wakati wa operesheni hiyo, utashuhudia makazi yake na barabara zikiwa kwenye hadhi ya miji iliyopangwa kitaalamu.

Upangaji wa miji na mengine yanayofanana na hayo, unahitaji wataalamu wa kufanya kazi hiyo.

Katika kuhakikisha nchi inakuwa watumishi wa eneo hilo wenye weledi, Chuo cha Ardhi Morogoro, taasisi ya elimu inayomilikiwa na serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imekuwa sehemu ya mikakati ya uandaaji wa wataalamu.

Mkuu wa Chuo hicho, Huruma Lugalla, anasema wanajivunia kipindi hiki ambapo taifa limefikisha miaka 60 ya uhuru kuajirika kwa wahitimu wa chuo chake.

Anabainisha kuwa ajira za wahitimu wa Chuo cha Ardhi Morogoro zipo katika maeneo mengi.

Waajiri wakuu ni wizara, idara na mashirika ya umma, mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri za majiji, miji na wilaya na kampuni binafsi ya upimaji na upangaji wa miji na vijiji.

Waajiri wengine pia ni kampuni za ujenzi wa majengo na barabara, viwanja vya ndege, reli, bandari, bomba la mafuta, mabwawa na njia za usambazaji umeme na maji.

"Tunapata faraja kubwa kuona wengi wa wahitimu wetu wakishiriki katika miradi mikubwa ya kimkakati kupitia sekta ya umma na sekta binafsi," anasema.

Lugalla anasema Chuo cha Ardhi Morogoro kimekuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa malengo, sera na mipango mbalimbali ya serikali.

Zainab Hussein, mkazi wa Morogoro, anakipongeza chuo hicho kwa kufundisha vijana kozi zinazowawezesha wahitimu kupata ajira na hivyo kuchangia kwenye ukuaji wa Pato la Taifa.

"Chuo kimekuwa moja ya nembo au taswira nzuri kwa mkoa wetu wa Morogoro," anapongeza.

Mkuu wa Chuo hicho (Lugalla) anasema kwa sasa wanatoa mafunzo katika fani mbili, ambazo ni upimaji na ramani (Geomatics) na fani ya mipangomiji na vijiji (Urban and Regional Planning).

### FANI MOJA

Anafafanua kuwa mwanzoni chuo kilikuwa kikitoa mafunzo ya fani moja tu ambayo ni Upimaji na Ramani (Land Surveying) kwa ngazi ya astashahada (certificate). Mafunzo hayo yalikuwa yakitolewa kwa muda wa miezi sita.

Mwaka 1979 mafunzo hayo yalibadilishwa kutoka miezi sita na kuwa ya mwaka mmoja. Mabadiliko zaidi yalifanyika mwaka 1983, ambapo mafunzo ya fani ya Upimaji na Ramani kwa ngazi ya astashahada yalibadilishwa na kuwa ya miaka miwili.

Anabainisha kuwa mafunzo ya stashahada ya upimaji yalianzishwa mwaka 2001, ili kuongeza fursa ya wahitimu kujiendeleza zaidi kitaaluma katika ngazi ya shahada. Mafunzo haya pia yalilenga kuzalisha mafundi sanifu katika ngazi ambayo inahitaji usimamizi mdogo kwenye utendaji wa kila siku.

Anasema Chuo cha Ardhi Morogoro kilipata ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) mwaka 2009 na kimeanzisha mtaala mpya wa mafundi sanifu wa fani ya Mipango Miji na Vijiji tangu mwaka wa masomo wa 2018/19.

Mkuu huyo wa Chuo anayataja mafanikio kwa kuangalia viashiria vya mafanikio, kama vile ongezeko la udahili wa wanafunzi, ongezeko la kozi zinazofundishwa, kuajirika kwa wataalamu wanaozalishwa na chuo na mchango wa wahitimu katika ustawi wa taifa.

Anabainisha kuwa chuo kipo katika maandalizi ya kuanzisha mitaala ya fani nyingine kama ilivyofafanuliwa katika Mpango Mkakati wa Chuo wa 2016/17 - 2021/22. Ongezeko hilo linaendana na matakwa ya Sheria ya Chuo cha Ardhi Na. 35 ya Mwaka 1974.

Anasema kimefanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kutoka wanafunzi 61 mwaka wa masomo 2008/09 na kufikia wanafunzi 554 mwaka wa masomo 2020/21.

"Katika mwaka wa masomo wa 2021/22, idadi ya wanafunzi waliosajiliwa ni 501 ambapo wavulana ni 346 (asilimia 69) na wasichana ni 155 (asilimia 31).

Anasema kozi ya Mipangomiji iliyoanzishwa mwaka 2018 imekuwa na mafanikio makubwa ambapo mpaka sasa kuna wahitimu 33 wa ngazi ya stashahada (Diploma in Urban and Regional Planning).

Baadhi ya kazi walizofanikisha ni upimaji wa viwanja vya makao makuu ya Wilaya za Mkinga (eneo la Kasera), Kilindi (eneo la Songe), Mvomero (eneo la Wami Sokoine), Chemba (mji wa Chemba), Kalambo (Mji wa Matai), Kyerwa (eneo la Rubwera) na Morogoro Vijijini (eneo la Mvuha).

Zingine ni upimaji wa viwanja vya makazi katika majiji ya Arusha (eneo la Burka na Lakilaki), Tanga (Kange, Kasera, Mwakidila, Pongwe, Mabokweni, Amboni, Pande), Dar es Salaam na Dodoma.

"Upimaji wa viwanja katika Halmashauri za Manispaa ya Iringa, Bukoba, Shinyanga, Moshi, Singida na Morogoro," anasema.

Kiongozi huyo anasema chuo kinatambua mahitaji ya sasa ya soko la nguvu kazi linalosukumwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika utendaji wa kila siku na kwa muktadha huo, kimefanya maboresho kadhaa ya mitaala, vifaa vya kufundishia na vitendea kazi.

Anasema kwa miaka arobaini (1978 - 2018), Chuo cha Ardhi Morogoro kilikuwa kikifundisha kozi moja tu, yaani Land Surveying.

Ili kunufaika na fursa za matumizi sahihi ya rasilimaliwatu na miundombinu, chuo kiliamua kuongeza kozi ya pili, yaani Urban and Regional Planning mwaka 2018.

"Maboresho haya yanaendana na Sera ya Elimu inayosisitiza kujiondoa katika mfumo wa kufundisha kozi moja na kufuata mfumo wa kozi zaidi ya moja," anasema.

### MIKAKATI YA CHUO

Anabainisha mikakati iliyopo sasa chuoni hapo inajumuisha kuendeleza eneo la ekari 32 lililoko Mlima Kola katika Manispaa ya Morogoro kwa lengo la kupunguza matatizo ya miundombinu.

Vilevile, anasema mipango yao inajumuisha kusomesha wakufunzi na wafanyakazi wengine katika ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu kwa lengo la kujenga uwezo wa kitaaluma.

Anabainisha kuwa Chuo cha Ardhi Morogoro kina seti tatu ya vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi kwa njia ya satelaiti (GNSS Receivers) vinavyotumika kufundishia na kufanya kazi za ushauri wa kitaalamu.

# NDUGAI AICHOMOA TIMU YA BUNGE MICHUANO YA EALA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BUNGE la Tanzania, limejitoa katika mashindano ya michezo mbalimbali ya Mabunge ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kutokana na hujuma wanazofanyiwa na Wabunge wa Uganda.

**Akitangaza uamuzi huo wa kujitoa jana jijini Arusha, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema amefikia uamuzi huo baada ya timu ya mpira wa pete ya Uganda, kususa kucheza na timu ya Bunge la Tanzania, kwa kuwakataa wachezaji wawili ambao ni watumishi wa Bunge.**

Ndugai, ambaye alikuwa uwanjani hapo tangu saa 3:30 asubuhi kwa ajili ya kushuhudia mchezo huo, alishangazwa na malumbano na vurugu zilizosababishwa na Uganda juu ya Tanzania.

"Kama katika mchezo huu wanadai Tanzania tumechezesha wachezaji wawili ambao si wabunge, lakini sheria inasema katika mpira huu wabunge watano na wawili watumishi wa bunge na tumeifuata ila wao hawataki," alisema.

Baada ya kauli hiyo, Spika Ndugai aliziita timu zote za Bunge la Tanzania na kuziagiza kuingia ndani ya magari kurejea Dodoma, jambo ambalo wabunge wote walitii na kuondoka eneo la uwanja huo.

Alisema lengo la michezo hiyo ni kuimarisha mahusiano, lakini anaona kwa wenzao hao wanaleta vurugu na malumbano, hivyo hawaelewi lengo lao ni lipi.

Aidha, baada ya kumaliza kuzungumza na wabunge wake, alimpa taarifa Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Dk. Martin Ngoga, ambao ni waandaaji wa michuano hiyo, kuwa timu za wabunge wa Tanzania zimejiondoa katika mashindano hayo.

Spika Ngoga alimsihi Ndugai kuvuta subira kwa sababu michezo iliyobaki ni michache, jambo ambalo Ndugai alisema hawapo tayari kuendelea na michezo hiyo ambayo mingi wameshinda na kwamba watakutana wakati mwingine.

Meneja wa timu za Bunge la Tanzania ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Manonga, Seif Gulamali, alisema Uganda wanatoa hoja zisizo na mashiko kwa sababu sheria ya mpira wa pete inataka wabunge watano na watumishi wawili wa bunge ambao ndio waliowaleta uwanjani.

"Lakini si tu kuwaleta leo hawa wamecheza mechi za mashindano kama haya kwa miaka mitatu mfululizo kwenye nchi ya Uganda na Kenya na hawakuwakataa, iweje mwaka huu wawakatae," alihoji.

Alisema wachezaji wa timu za Bunge la Uganda wamekuwa wakileta vurugu mara kwa mara dhidi ya timu za Tanzania ambapo juzi waziri wa michezo wa nchini hiyo alimpiga muamuzi wa mechi ya soka kati ya Tanzania na Uganda na kusababisha mchezo huo kuvunjika," alisema.

Gulamali alisema pamoja na vurugu hizo, lakini mwenyekiti wa michezo hiyo ambaye ni Mbunge wa Bunge wa EALA, Suzan Nakawuki, ameshindwa kusimamia mashindano hayo kwa sababu ametoka Uganda na muda wote ameonekana akizibeba na kutetea nchi yake hata kama wameonekana wakifanya makosa.

Michezo hiyo ambayo ilianza Desemba 6, mwaka huu kwa kuzinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ilitarajiwa kufikia kilele chake kesho, Ijumaa.



Timu ya mpira wa pete ya Bunge Tanzania katika picha ya pamoja na Spika Job Ndugai (wa pili kushoto waliosimama), akiwatakia kila la kheri muda mfupi kabla ya kuchuana jana na timu ya wabunge wenzao kutoka Uganda katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana, hata hivyo mechi hiyo haikuchezwa baada ya Wabunge wa Uganda kuleta vurugu. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Kidunda sasa ajigamba kumchapa Mkongomani

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Selemani Kidunda, amesema amejianda vizuri kuelekea kulipa kisasi kwa mpinzani wake kutoka DR Congo, Tshimanga Katompa, katika pambano litakalofanyika Desemba 26, mwaka huu, katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kidunda alisema anataka kuonyesha ulimwengu na Watanzania kuwa hakuna bondia anayeweza kuja kushinda ndani ya ardhi ya Tanzania.



Alisema anafanya mazoezi kuweka mwili wake kamili dhidi ya mpinzani wake huyo na kuwaonyesha Watanzania kwamba wanaenda kupambana kutafuta ushindi mbele ya Mkongomani huyo.

"Nimejiandaa vizuri na sasa tusubiri siku ya pambano ifike na hatatoka na ushindi wowote, kwa sababu ya mazoezi mazuri na kujiimarisha zaidi kwa qjili ya mpinzani wangu huyo na nitampiga Kamtopa kwa namna yoyote, kwa staili yoyote hatatoka, kikubwa ni sapoti kutoka kwa Watanzania,"alisema Kidunda.

Mbali na pambano hilo, pia kutakuwa na mapambano mengine ambapo; Ismai Galiatano atapanda ulingoni dhidi ya Denis Mwale, Ibrahim Class dhidi ya Israel Kamwamba, George Bonalacha na Hassan Milanzi, Pali Magesta na Oscar Richard huku Viguli Shafii akiwa na kazi pevu dhidi ya Ally Kilongola.

Wengine ni Hamis Kibodi dhidi ya Iddy Jumanne, Grace Mwakamela na Ruth Chisale, Najma Isike na Leila Zayidu na Daniel Materu dhidi ya Haruna Swanga.

# Nado nje Azam FC msimu mzima

**Adam Fungamwango na**

**Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC kimezidi kukumbwa na majeruhi wa muda mrefu, baada ya mchezaji wake tegemeo, Idd Selemani 'Nado' kuumia goti na hatoonekana tena uwanjani kwa msimu wote uliosalia wa 2021/22, hadi Septemba mwakani.

Akizungumza kutoka Afrika Kusini, Daktari Mkuu wa klabu hiyo, Mwanandi Mwankemwa amesema mchezaji huyo anatarajiwa kufanyiwa operesheni ya goti la kulia na atakuwa nje ya dimba kwa miezi tisa.

Nado aliumia kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kati ya timu hiyo na Mtibwa Sugar iliyopigwa Novemba 30, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi na wenyeji kushinda bao 1-0.

"Tumefika salama Afrika Kusini na mgonjwa, tumekutana na daktari Nicolaus, mchezaji ameumia goti la kulia, matibabu yataanza Ijumaa (kesho) kwa vipimo vya maabara vya ugonjwa wenyewe yaani goti na COVID-19, operesheni yenyewe itafanyika Jumatatu," alisema daktari huyo.

Aliongeza kuwa baada ya kufanyiwa operesheni Nado atatakiwa kufanya mambo kadhaa, ikiwamo mazoezi ya kuendesha baiskeli na kukimbia.

"Siku chache baada ya operesheni ataanza mazoezi ya kuendesha baiskeli kwa wiki tatu, halafu baada ya hapo, ataanza mazoezi ya kukimbia kwa muda wa wiki sita. Ni kwamba hatorejea tena uwanjani mpaka baada ya miezi tisa. Tupo hata hadi Desemba 24 na Desemba 25 tutarejea nchini Tanzania," alisema daktari huyo.

Kuumia kwa Nado ni pigo kubwa kwa Azam ambayo kwa sasa haifanyi vema kwenye Ligi Kuu, huku pia ikiendelea kumkosa straika wake hatari Prince Dube, ambaye mbali na kuwa majeruhi wa mara kwa mara, lakini mara ya mwisho aliumia wakati wa maandalizi ya msimu huu wa ligi.

## ZISIKUPITE

### DELE HUYOOO NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle wamefanya ufuatiliaji wa awali kuhusu Dele Alli, huku Tottenham wakiwa tayari kusikiliza ofa kwa kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 25. ***(Teamtalk)***

### POGBA 'BAIBAI' UNITED

MANCHESTER United wanaangalia timu inayomtaka Paul Pogba mwenye miaka 28, akitarajiwa kuondoka bure wakati mkataba wa kiungo huyo wa kati wa Ufaransa utakapokamilika msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### BARCA JICHO KWA MAATSEN

KLABU ya Barcelona wanapanga mpango wa kumnunua beki wa kushoto wa Chelsea, Mholanzi Ian Maatsen mwenye miaka 19, ambaye yuko kwa mkopo wa msimu mzima na klabu ya Championship Coventry.***(Football Insider)***

### MARTIAL KUTUA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid wanataka kutazama uwezekano wa kufanya makubaliano na Manchester United kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26. ***(Eurosport)***

### MILENKOVIC ATAJWA WEST HAM

WEST Ham pia wana matumaini ya kumnunua, Nikola Milenkovic kama makubaliano kati ya mlinzi huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 24, na mmiliki wa Fiorentina yanamaanisha kuwa huenda akahama. ***(Teamtalk)***

### PHILLIPS KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inajiandaa kusonga mbele kwa kutaka kumnunua Nat Phillips wa Liverpool Januari, licha ya kuwa na jeraha la hivi majuzi la beki huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 24. ***(Standard)***

### VLAHOVIC BEI JUU

KLABU ya Fiorentina wameweka bei ya euro milioni 100 kwa mshambuliaji wao wa Serbia, Dusan Vlahovic, 21.***(Gazzetta Sport)***

### LINGARD YUPO SANA UTD

MANCHESTER United haitarajii Jesse Lingard kuondoka katika dirisha la uhamisho la Januari, huku kiungo huyo wa kati wa Uingereza mwenye umri wa miaka 28, akikaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake.***(Manchester Evening News)***

### CASTELLANOS AFUATILIWA

WEST Ham inamfuatilia mshambuliaji wa Argentina na New York City, Valentin Castellanos, 23. ***(Mail)***

### AIT-NOURI AGOMBEWA

KLABU za Paris St-Germain, Barcelona, Liverpool, Manchester City na Tottenham zote zinafikiriwa kumfuatilia mlinzi wa kushoto wa Ufaransa, Rayan Ait-Nouri mwenye umri wa miaka 20, lakini Wolves watapokea asilimia 50 pekee ya ada yoyote ya uhamisho kutokana na kifungu cha mauzo. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG AANZA KUFUNGULIWA MLANGO

**Chochote kitakachotokea katika chumba cha maandalizi siwezi kusema ukiukaji huo...**

**LONDON,** England

ARSENAL wamempokonya unahodha wa timu hiyo, mshambuliaji wao, Pierre Emrick Aubameyang baada ya kukosa nidhamu.

**Mshambuliaji huyo wa Gabon, ambaye hakushirikishwa katika mechi ya Jumamosi, ambayo Arsenal ilishinda mabao 3-0 dhidi ya Southampton, pia hakushirikishwa katika mechi dhidi ya West Ham, jana Jumatano.**

"Tunataraji wachezaji wetu wote hususan nahodha wetu , kufuata sheria na viwango vilivyowekwa na kukubalika," ilisema taarifa ya Arsenal.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, aliachwa nje kwa makosa ya kinidhamu Machi mwaka huu.

Wakati huo, alikosa ushindi dhidi ya wapinzani wao Tottenham kwa kukiuka itifaki ya kabla ya mechi.

Wakati huu kocha wa klabu hiyo, Mikael Arteta hajasema ni vipi Aubameyang alivunja sheria hiyo, lakini mchezaji huyo amesema kwamba, alirudi akiwa amechelewa kutoka safari ya ughaibuni.

"Tumekuwa tukisisitiza kwamba kuna makubaliano ambayo hayawezi kukiukwa katika klabu hii," alisema Arteta baada ya mechi ya Southampton.

"Chochote kitakachotokea katika chumba cha maandalizi siwezi kusema. Upande wangu siwezi kusema ukiukaji huo ulikuwa wa aina gani."

Aubameyang alichukua wadhfa wa nahodha Novemba 2019, baada ya kiungo wa kati, Granit Xhaka kupokonywa nafasi hiyo na aliyekuwa kocha, Unia Emery.

Aubameyang ambaye alijiunga na Arsenal kwa dau la pauni milioni 56, kutoka klabu ya Borussia Dortmund ya Ujerumani, alitia saini ya mkataba wa miaka mitatu mwaka uliopita.

Msimu huu amefunga mabao manne katika mechi 14 za Ligi Kuu England na hajafunga tangu Oktoba 22, mwaka huu.

## HABARI MICHEZO







# PSG, REAL MADRID ZAMWANIA RUDIGER



**LONDON,** England

KLABU ya PSG ya nchini Ufaransa hivi karibuni itafungua mazungumzo baada ya Real Madrid kuripotiwa kutaka kumsajili beki kisiki wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, wakati huu mkataba wake na klabu hiyo ya London ukikamilika mwishoni mwa msimu.

Kwa mujibu wa Jarida la BILD, Rudiger amekataa mkataba mpya uliowekwa mezani na Chelsea, baada ya kumpa mshahara wa Euro 140,000 kwa wiki wakati mchezaji huyo akitaka Euro 200,000 kwa wiki.

Taarifa zinaeleza kuwa wakala wa mchezaji huyo ameshafungua mazungumzo na Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo kwa ajili ya usajili wa beki huyo.

Rudiger ambaye anaingia katika miezi 6 ya mwisho ya mkataba wake, pia amehusishwa na klabu ya Real Madrid, Barcelona na Manchester United ambazo zimeonyesha nia endapo atashindwa kuongeza mkataba.

Antonio Rudiger amedumu Chelsea kwa miaka mitano akiwa ameisaidia timu hiyo kutwaa Kombe la FA, Europa League na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Barcelona hawajakata tamaa kwa Haaland

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema anaangalia namna ya kutafuta njia ya kuipata saini ya mshambuliaji wa Dortmund, Erling Haaland.

Licha ya changamoto za kifedha katika klabu ya Barcelona, lakini wapo tayari kumwaga fedha ya kutosha kwa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Norway, kwani iko wazi kwamba Barca wanatatizo katika eneo la ushambuliaji kwa kushindwa kupata idadi kubwa ya mabao kwenye mechi zao.

Kwa tishio lake la kushambulia, umri wake na wasifu wake, Barcelona wanamwona Haaland kama chaguo bora, mchezaji ambaye wanaweza kuona faida kubwa, ndani na nje ya uwanja. Sehemu ngumu, bila shaka, itakuwa kukamilisha dili hiyo.

Kuna uvumi mkubwa unaoendelea kwamba Haaland anaweza kupatikana mwisho wa msimu, lakini dau bado inasemekana kuwa linacheza kwenye euro milioni 70. Halafu, kuna mshahara wa mchezaji na ada ambayo wakala wake, Mino Raiola ataafiki.

Laporta hajaonyesha dalili zozote za kukata tamaa na ataendelea kuwinda saini ya mchezaji huyo nyota wa Bundesliga mpaka mwisho.



HABARI MICHEZO





# 3,781,040 JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/12/2021 | 18:00 | Bristol City vs Huddersfield | 2.69 | 3.18 | 2.54 |
| 02. 18/12/2021 | 18:00 | Watford vs Crystal Palace | 2.89 | 3.34 | 2.41 |
| 03. 18/12/2021 | 20:30 | Leeds vs Arsenal | 2.97 | 3.41 | 2.32 |
| 04. 18/12/2021 | 22:45 | Cagliari vs Udinese | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 05. 18/12/2021 | 23:00 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 06. 19/12/2021 | 15:00 | Everton vs Leicester | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 19/12/2021 | 16:00 | Granada vs Mallorca | 2.49 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 19/12/2021 | 16:00 | Fuenlabrada vs Real Oviedo | 2.90 | 3.05 | 2.45 |
| 09. 19/12/2021 | 17:00 | Spezia vs Empoli | 2.40 | 3.49 | 2.79 |
| 10. 19/12/2021 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.79 | 3.44 | 2.40 |
| 11. 19/12/2021 | 18:00 | Zaragoza vs Tenerife | 2.38 | 3.08 | 2.98 |
| 12. 19/12/2021 | 20:30 | Getafe vs Osasuna | 2.49 | 2.90 | 3.20 |
| 13. 19/12/2021 | 22:45 | AC Milan vs Napoli | 2.37 | 3.41 | 2.91 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 16 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3258 | Umraniyespor vs Bursaspor | 1.74 | 3.61 | 4.05 |
| 14:30 | 5277 | Jiangxi Liansheng vs Zibo Sunday | 2.17 | 3.33 | 2.95 |
| 15:00 | 3385 | Hadiya Hosahina FC vs Dire Dawa Kenema FC | 2.63 | 2.83 | 2.73 |
| 15:00 | 3898 | FK Graficar Beograd vs FK Loznica | 3.41 | 3.37 | 1.96 |
| 15:30 | 1543 | Sabayil vs Sabah | 3.71 | 3.08 | 1.98 |
| 16:00 | 3094 | Chindia Targoviste vs U Craiova SA | 2.29 | 2.85 | 3.43 |
| 16:00 | 4686 | Proleter vs Radnicki Nis | 2.60 | 3.03 | 2.60 |
| 17:00 | 3583 | Shabab AL Amari vs Mosaset AL Bireh | 3.97 | 3.29 | 1.84 |
| 17:00 | 4546 | Ittihad Kalba vs Jazira Abu Dhabi | 2.89 | 3.27 | 2.23 |
| 17:00 | 4984 | Bengaluru FC vs ATK Mohun Bagan | 2.74 | 3.23 | 2.35 |
| 17:30 | 5902 | Arda Kurdzhali vs CSKA Sofia | 4.13 | 3.41 | 1.77 |
| 18:00 | 1586 | Primeiro De Agosto vs Wiliete SC | 1.67 | 3.22 | 5.20 |
| 18:00 | 3504 | OFI Crete vs Aris Salonica | 2.85 | 3.34 | 2.35 |
| 18:00 | 4480 | Addis Ababa City FC vs Hawassa Kenema SC | 3.95 | 2.85 | 2.20 |
| 18:00 | 4664 | Karabakh vs Zira | 1.48 | 3.86 | 5.98 |
| 18:05 | 1268 | Backa Topola vs Red Star Belgrade | 9.69 | 5.43 | 1.23 |
| 18:30 | 1981 | CS Mioveni vs Dinamo Bucuresti | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 19:00 | 3341 | Stella Club dâ€™Adjame vs ASEC Mimosas | 7.16 | 3.97 | 1.41 |
| 19:00 | 5056 | Adanaspor vs Istanbulspor | 2.70 | 3.27 | 2.36 |
| 19:10 | 1864 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 1.82 | 3.95 | 3.37 |
| 19:15 | 5794 | Al Nasr Dubai vs AL Wahda Scc (UAE) | 1.83 | 3.47 | 3.76 |
| 20:00 | 2761 | Spezia vs Lecce | 2.06 | 3.55 | 3.25 |
| 20:00 | 2789 | Al Hilal Riyadh vs Al Nasr Riyadh | 1.87 | 3.52 | 3.97 |
| 20:00 | 5342 | Cambuur vs NEC Nijmegen | 1.98 | 3.41 | 3.32 |
| 20:30 | 4046 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.09 | 8.12 | 16.43 |
| 20:30 | 4394 | Ionikos Nikea FC vs AEK Athens | 6.32 | 4.15 | 1.48 |
| 20:35 | 2670 | AS Ashdod vs FC Ahva Kfar Manda | 1.25 | 5.05 | 9.70 |
| 20:45 | 2424 | Hapoel Haifa vs Hapoel Kfar Saba | 1.47 | 4.04 | 5.77 |
| 20:45 | 5117 | Hapoel Raanana W vs Bnot Netanya W | 1.70 | 4.04 | 3.80 |
| 20:45 | 5291 | Royal Antwerp vs Eupen | 1.59 | 4.23 | 4.72 |
| 21:00 | 1394 | CD Arenteiro vs Valencia | 16.76 | 7.10 | 1.14 |
| 21:00 | 1643 | Hapoel Petah Tikva vs Maccabi Netanya | 4.63 | 3.43 | 1.69 |
| 21:00 | 2010 | Amorebieta vs Almeria | 3.20 | 3.25 | 2.20 |
| 21:00 | 4002 | UD Llanera vs Mallorca | 18.76 | 7.50 | 1.13 |
| 21:30 | 2282 | Farul Constanta vs CFR Cluj | 3.87 | 3.09 | 2.01 |
| 21:30 | 4997 | TSG Sprockhovel vs SG Wattenscheid | 3.48 | 4.15 | 1.75 |
| 22:00 | 1427 | Lugo vs Mirandes | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 22:00 | 1579 | Achilles Veen vs DVS 33 Ermelo | 5.19 | 3.94 | 1.53 |
| 22:30 | 1714 | Leicester vs Tottenham | 2.17 | 3.55 | 3.15 |
| 22:45 | 3230 | Chelsea vs Everton | 1.23 | 6.02 | 12.03 |
| 23:00 | 2092 | Albacete Balompie vs Cadiz CF | 4.95 | 3.96 | 1.61 |
| 23:00 | 2231 | Sampdoria vs Torino | 2.40 | 3.36 | 2.77 |
| 23:00 | 2357 | Atletico Baleares vs Getafe | 4.43 | 3.64 | 1.74 |
| 23:00 | 2883 | Deportivo La Coruna vs Osasuna | 4.34 | 3.65 | 1.75 |
| 23:00 | 2910 | Valenciennes vs Strasbourg | 3.74 | 3.30 | 1.98 |
| 23:00 | 4082 | Liverpool vs Newcastle | 1.12 | 8.97 | 18.94 |
| 23:00 | 4715 | Atl Mancha Real vs Granada | 21.70 | 8.09 | 1.10 |
| 23:00 | 5199 | Heerenveen vs De Treffers | 1.10 | 8.08 | 15.40 |
| 23:00 | 5230 | Racing Genk vs Charleroi | 1.93 | 3.75 | 3.46 |
| 23:15 | 2344 | Boavista vs Sporting Braga | 4.35 | 3.86 | 1.72 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# RASMI AGUERO ASTAAFU SOKA




**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Sergio Kun Aguero, jana Jumatano ametangaza kustaafu soka rasmi kutokana na tatizo la moyo.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 33, amesema, amechukua maamuzi hayo kwa kuheshimu ushauri wa kiafya aliopewa na madaktari wa FC Barcelona ambao wamekuwa wakimuangalia tangu alipogundulika na tatizo la moyo.

Aguero alisema: "Huu mkutano ni maalumu kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe kwamba nimeamua kusimama kucheza mpira. Ni wakati mgumu na maamuzi ambayo nimeyachukua ni kwa ajili ya afya yangu, hii ni sababu kubwa."

Aguero alianza kupata maumivu katika mchezo dhidi ya Alaves uliomalizika kwa sare ya bao 1-1 Oktoba, mwaka huu.

Ikumbukwe kwamba Aguero alijiunga na FC Barcelona msimu huu akiwa mchezaji huru kwa dili la miaka miwili akitokea Manchester City ambapo huko aliweka rekodi ya kuwa mzee wa kutupia katika misimu 10 ambayo amecheza.

City ilipata saini ya Aguero 2011 akitokea Klabu ya Atletico Madrid na aliweza kufunga bao la maajabu katika msimu wa 2011/12 na kuipa timu hiyo taji la kwanza la Ligi Kuu England.

# Mayele alia mabeki kumpania

**Na Dennis Fussi**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, Fiston Mayele, amesema sababu ya yeye kushindwa kuifungia bao timu yake kwenye mchezo dhidi ya Simba ni kutokana na mabeki wa timu hiyo kumpania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mayele amesema yeye na wenzake walijitahidi kupambana na kutengeneza nafasi kadhaa za mabao, lakini ilishindikana kutokana na mkakati ambao uliwekwa na wapinzani wao, Simba.

"Ulikuwa mchezo mgumu hasa kwangu kwa sababu jamaa walinikaba kupita kiasi, sikuwa na muda hata wa kufanya kile nilichokusudia, lakini ndio mchezo wa mpira unavyokuwa," alisema Mayele.

Aliongeza kusema kuwa, kwa sababu yeye ameonekana kuwa tishio, walinzi wa Simba waliingia kwenye mchezo huo wakiwa wamempania sana.

Katika mchezo huo Mayele alidhibitiwa vilivyo na mabeki Joash Onyango na Henock Inonga 'Varane'.



# Michezo

Alhamisi Desemba 16, 2021

Nipashe




Aubameyang afunguliwa mlango

UKURASA 21

KIMOJA TU...



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kushoto), akishangilia sambamba na Pape Sakho baada ya kuifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya JKT Tanzania katika mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**

# Simba yatoa sababu ya ushindi kiduchu

●●● Kocha asema kazi sasa itaanza dhidi ya Kagera Sugar Jumamosi, wakwea pipa kuifuata...

**Saada Akida na Adam**

**Fungamwango**

BAADA ya kuambulia ushindi mwembamba wa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, ametaja sababu inayowafanya kushindwa kuibuka na mabao mengi katika michezo yao.

**Huku akikiri kucheza mechi hiyo kwa tahadhari kubwa kuhofia kilichowatoa miaka kadhaa nyuma, walipotolewa na timu za Green Warrios na Mashujaa FC, Matola alisema tatizo kubwa ni safu yao ya ushambuliaji kushindwa kutumia nafasi wanazotengeneza.**

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na Simba kuondoka na ushindi wa bao 1-0, Matola alisema kwanza kabisa walichezesha wachezaji ambao walikuwa hawatumiki sana kwenye mechi za nyuma na kuwapumzisha wengi wa kikosi cha kwanza kutokana na timu yao kuwa na ratiba ngumu, lakini pia walichotaka kwenye mechi hiyo ni ushindi kwa sababu ilikuwa ni mechi ya mtoano, hivyo waliingia kwa tahadhari kubwa.

"Tumekuwa na tatizo la kushindwa kutumia nafasi za mwisho, tumeliona hilo na tutalifanyia kazi kuhakikisha mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar halijitokezi tena," alisema Matola.

Kikosi cha Simba ambacho kinatarajiwa kuondoka leo kuelekea Bukoba mkoani Kagera, kitashuka Uwanja wa Kaitaba mjini humo Jumamosi wiki hii kuvaana na wenyeji, Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara.

"Tangu tulivyocheza na Red Arrows (Kombe la Shirikisho Afrika), zimepita siku 10 na baada ya hapo tukacheza mechi kubwa dhidi ya Yanga, tulitumia nguvu nyingi na kila baada ya siku mbili tunacheza.

"Hivi tunavyozungumza, Desemba 18, mwaka huu [Jumamosi], tunacheza mechi dhidi ya Kagera Sugar, mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lazima mabadiliko ya mara kwa mara ya kikosi yatokee," alisema Matola huku akiwapongeza wachezaji wao kwa ushindi huo.

Kuhusu ugumu wa michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho nchini, Matola alisema: "Siku zote michezo ya mtoani inakuwa migumu sana, utakumbuka miaka kadhaa nyuma tuliwahi kucheza na timu kama hizi na zikatutoa, tena tukiwa na wachezaji wetu wote mastaa wakubwa."

Mwaka 2017, Simba ilitolewa na timu ya Ligi Daraja la Pili, Green Warriors kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na mwaka uliofuata ilitolewa kwenye michuano hiyo kwa kufungwa mabao 3-2 dhidi ya Mashujaa ya Kigoma iliyokuwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Abdallah 'Bares' alisema kuwa waliidhibiti Simba katikati ya uwanja kama ilivyokuwa mpango na mkakati wao, lakini safu yake ya ushambuliaji ikamwangusha.

"Lengo lilitimia, ilikuwa ni kudhibiti sehemu ya kiungo na tulifanikiwa, lakini washambuliaji wangu hawakuwa makini, naipongeza Simba, kwa sababu wao ni mabingwa watetezi, nawatakiwa kila la kheri kwenye michuano hii," alisema.

## Ndugai aitoa Bunge michuano ya EALA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BUNGE la Tanzania, limejitoa katika mashindano ya michezo mbalimbali ya Mabunge ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki...



HABARI UK.20

## Real Madrid, PSG zamwania Rudiger

**LONDON,** England

KLABU ya PSG ya nchini Ufaransa imekuwa ya hivi karibuni kufungua mazungumzo baada ya Real Madrid kuripotiwa kutaka kumsajili beki...



HABARI UK. 22

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >